

YUPO MTU HAPA ANAYEWEZA KUIWASHA TAA

 . . . tuinamishe vichwa vyetu sasa. Baba wetu wa mbinguni, tunakushukuru asubuhi hii kwa wema na rehema Zako, kwa kutujalia tukusanyike hapa tena—siku moja upande huu wa ile milele kuu—kumuabudu Yeye aliye mzuri sana, Bwana Yesu Kristo. Tunakushukuru Wewe kwa sababu Yeye alikuja duniani ku—kutukomboa sisi kutokana—na—na maisha ya dhambi na kutupa sisi urithi huu mkuu tulio nao kwa haki Yake. Na kama sisi, asubuhi hii, tulivyo hapa kama mabalozi Wake ku—kuumega huu Mkate wa Uzima kwa kusanyiko hili linalongoja, hebu Roho Mtakatifu aongoze kila neno na kuliweka mioyoni mwa watu sawasawa na haja zetu. Twaomba hili katika Jina la Yesu. Amina. (Ketini.)

² Hakika nayahesabu haya kuwa majaliwa makubwa tena asubuhi hii kusimama hapa pamoja nanyi. Nasikitika kwa vile hatuna nafasi zaidi kuliko tuliyo nayo kwa kuwashughulikia watu; maskani yetu si makubwa kutosha. Na tunashukrani nyingi kuwa hapa katika likizo kuu hizi kutoka—kutoka chini kule nyumbani kwetu katika—kule Tucson. Na hali ya hewa ilikuwa baya, lakini tulifurahia kuwa hapa na kufanya mkutano.

Sasa, ninataka kutangaza kuwa usiku huu kutakuwa na ibada ya uponyaji usiku huu au maombi kwa ajili ya wagonjwa. Na ni—nimemwambia Billy sasa hivi. . . Akasema, “Vema, utafanyaje?”

³ Nikasema, “Naam, pengine ni afadhali uwape kadi kadha usiku huu yapata saa 12:30, ili watu wasi. . . Na mwaona, kumejaa sana hapa, tunaweza kujua tu namna ya kuwaleta mmoja mmoja ili uweze kuitwa kwa nambari ya kadi yako, na hivyo kusiwe na msongamano. Tunaweza kuwaita tu mmoja mmoja na kuwapisha katika mstari tunapowaombea.

⁴ Basi u. . . Kama u mgonjwa au una wapenzi walio wagonjwa na wataka kuwaingiza, njoo kama saa 12:30, wakati kama huo, saa 1:00, na upate kadi ya maombi. Atakuwa mlangoni—au vile atakavyowapa—mnapoingia.

⁵ Na ndipo, pengine hii itakuwa nafasi ya mwisho nitakayopata kuwa hapa kwa muda fulani, kwa sababu nina shughuli nyingi sana sasa. Lakini sasa, bado ningali Marekani mpaka mwisho wa majira ya kati ya baridi na kiangazi. Kwa hivyo tu—pengine tutarudi baada ya kitambo kidogo katika majira ya kiangazi. Bwana akipenda, ningependa kufanya hivyo,

tukipata ma—mahali hapa kama hewa yake inabaridishwa. Nilikuwa nimuulize Billy; ningependa kuzungumza juu ya zile Baragumu Saba, niwe na mkutano hapa kwa zile Baragamu Saba yakiwa—yakiwa ni mapenzi ya Bwana. Kwa kuwa hizo ni—zile Nyakati Saba za Kanisa, na zile Muhuri Saba, na sasa zile Baragamu Saba. Na kama utapata nafasi kama Juni wakati watu wako likizoni, tuwapatie muda ili waweze—waweze kuingia.

⁶ Na nina furaha kumwona Ndugu Shepherd hapa asubuhi hii, mimi—kutoka katika hospitali hii. Nilienda kumwona juzi. Na Dada Shepherd, sikukupigia simu jana. Ile ndoto uliyonitumia ilikuwa nzuri sana, sana. Uiona, kama ilivyokuwa, Kristo katika—juu ya—katika—katika anga, juu ya huyu farasi mweupe, lakini angali amefungwa. Waona? Lakini hata hivyo, kabla haijatoweka, jamaa yako wote wakapata kuiona. Hiyo tafsiri ya ndoto ni kwamba jamaa yako wameona mwenendo Wake wa siku hizi za mwisho kabla haujakwisha kwa njia yoyote. . . Basi ni—ilikuwa ya kiroho kabisa, na baraka nzuri mno kwako—jamaa yako. Ile jamaa imetoka katika dhiki kuu kufikia walipo sasa.

⁷ Na sasa, tuko na jambo la kuhuzunisha kidogo asubuhi hii. Tangu nilipokutana hapa, na mmoja wa marafiki wetu wa dhamani na—na mmoja wa wanaohudhuria maskani haya, jamaa ya Coats, ambao sote tunawapenda. Wanatoka kule mashariki na—au kutoka karibu na Chicago. Na Dada Billy Habib, na—na kuna Dada Armstrong na wasichana hao wote. Wao—nadhani hapo mbeleni walikuwa Wanazarini na wamemjia Bwana, na ni marafiki wa dhamani sana kwetu. Na Ndugu na Dada Coats, baba yao na mama yao, walikuwa njiani kurudi nyumbani kutoka kule magharibi, na mtu fulani akateleza barabarani na—na kumuua Dada Coats papo hapo. Na—na waliponiita niende kule ni—nikiwa Tucson, na nikasikia kuhusu hayo, nilikuwa nimeketi pale wakati ule ule na kopo la peremende ambazo dada yule alikuwa amenitengenezea zikiwa me—mezani. Na mwajua vile hilo lilinifanya kusikia. Bali ni—ninafikiri kuwa—nashukuru Bwana asubuhi hii kwamba haikumbidi huyo dada kupata maumivu. Alikuwa anazeeka, na haikumbidi kupata maumivu. Naye alienda nyumbani kuwa pamoja na Mungu.

⁸ Nilikuwa ninafikiri na kuzungumza na wasichana wake wawili, sasa hivi tu, mle chumbani. Ndugu Coats yuko hapa asubuhi hii; alivunjika mbavu kadhaa. Na nilimpigia simu hospitalini na pale alipokuwa amelazwa hospitalini kule Missouri, na mbavu zake zimevunjika na kadhalika, lakini alikuwa na ujasiri kweli, Mkristo wa kweli, akijua kuwa maskini malkia wake hajakufa; yu hai milele pamoja na Kristo. Unaona? Na kutakuwa na wakati wa kuunganika.

⁹ Ayubu alisema wakati mmoja, “Ee, laiti Wewe ungalinificha kaburini na kuniweka mahali pa siri mpaka hasira Yako ipite.”

¹⁰ Je, mwishatambua kwamba Mungu katika maumbile hufanya jambo lile lile? Kama vile utomvu ulio katika mti hapa juu, ukiyashikilia majani, na kabla majira ya baridi kuja, hasira imwagwayo duniani. . . Mwaona, wakati fulani dunia haikuwa na majira ya baridi. Na katika ule Utawala wa Miaka Elfu hakutakuwa na majira ya baridi tena. Mwaona? Basi ni hasira juu ya dunia. Ndipo wakati hayo yalipotendeka. . . Mnaona, kabla hasira haijaja, Mungu katika rehema Zake huupeleka ule utomvu chini kabisa katika—chini ya ardhi katika mizizi ya ule mti na kuuweka pale mpaka hasira ya baridi kuu imepita, halafu anaupandisha juu tena katika majira ya mwisho wa baridi. “Ee, laiti Wewe ungalinificha kaburini na kuniweka mahali pa siri mpaka hasira yako ipite.” Hayo ndiyo amemtendea dada yetu; hayo ndiyo awatendeayo Wakristo wote.

¹¹ Ndugu Coats, Mungu akubariki. Nina furaha sana kujua kuwa—kwamba Muhuri wa Mungu hudumisha katika saa ya shida. Ninajua anayopitia, kwa sababu nilipitia katika jambo kama hilo miaka mingi iliyopita. Lakini nina. . . Mmoja kwa mmoja hatuna budi kuuvuka huu mto mkuu, na mimi—na itakuwa wakati wangu mojawapo ya siku hizi na wakati wako mojawapo ya siku hizi. Bali kama Daudi alivyosema, “Sitaogopa mabaya, kwa maana Wewe upo pamoja nami. Gogo Lako na Fimbo Yako vyanifariji.”

¹² Sasa, kwa ukumbusho wa Dada Coats, dada wetu wa dhamani ambaye ameenda kwa Mungu, mimi. . . Kama ukumbusho mdogo kwake asubuhi hii, ningependa mkutano wasimame kwa muda kidogo tu. Hebu tuinamishe vichwa vyetu na tumfikirie mtu mmoja ambaye wakati mmoja siku chache tu zilizopita alitembea katika—katika maskani haya, aliyeingia na kutoka miongoni mwetu, akatuamkua kwa mkono, Mkristo mzuri, sasa yupo pahali pale ambapo Bwana aliniruhusu nipaone sio muda mrefu uliopita, akiwa mwanamke kijana tena akingoja jamaa yake wanaokuja.

¹³ Baba wetu wa mbinguni, tunakushukuru kwa kumbukumbu za Dada Coats. Ni dada mpenzi, na wa dhamani jinsi gani. Na sasa, wakati hufika ambapo tunamaliza kuishi muda tuliopangiwa, lazima tuvuke ule mto. Tunakushukuru kwa sababu haikumbidi—kuwa na maumivu. Lazima hapakuwa na chochote hapa dhidi yake cha kumfanya aumie; alienda tu moja kwa moja mikononi mwa Mungu katika kitambo kidogo tu.

¹⁴ Mume wake, watoto wake wako hapa asubuhi hii, Bwana, wamerudi kabisa katika wajibu wao. Jinsi tunavyokushukuru kwa ile imani hodari, imani ya baba zetu ambayo ingali hai, badala ya kifungo, mwali wa moto, na upanga. Tunakushukuru kwa hayo yote.

¹⁵ Ipumzishe nafsi yake ya dhamani, Bwana. Alikuwa dada yetu. Huzuni, matone na machozi yatiririka miyoni mwetu kwa

ajili ya kutokuweko kwake, lakini furaha inabubujika kutoka kwa yale matone ya machozi na kutujulisha kwa hakikisho la Neno Lako kuwa yuangali hai katika maisha ambayo hayatakufa kamwe. Na hapatakuwa na ajali mahali alipo sasa, ni kuwangoja tu wale wanakuja baadaye wajiunge naye.

¹⁶ Mbariki Ndugu Coats na uwabariki wale wasichana katika jamaa yake, Bwana, na wale wapenzi, na wote wampendao. Na siku moja, Baba, tunatumaini kukutana naye katika ng'ambo ile kuu ambako hakuna ugonjwa, huzuni, wala mauti. Mpaka wakati huo, tuhifadhi sote katika afya na tukiwa wazima, tukikutumikia na kuitazamia ile siku. Katika Jina la Yesu Kristo twaomba hili. Amina.

¹⁷ Hebu yule Roho Mtakatifu mkuu atuhudumiaye hapa maskanini katika kulifunua Neno Lake, hebu na aipumzishe nafsi yake hodari katika amani hadi tutakapokutana naye.

¹⁸ Sasa, pana joto hapa ndani asubuhi hii, kwa maana ni—miili, mwajua, ikiwa nyingi sana—joto la mwili wa mwanadamu.

¹⁹ Sasa, tungependa kutoa tangazo sasa. Wakati mwingine ibada zetu hapa, huwa ndefu—asubuhi, sababu yake ni, hakika si vizuri kuwa na ibada ndefu hivyo, kwa sababu—saa moja, saa moja na nusu, wakati mwingine saa mbili. Bali kile ninachofanya, ninainasa kwa kanda hapa. Unaona? Na kanda hii inaenda dunia nzima. Na hiyo ndiyo mimi—tunakutana muda mrefu hivyo asubuhi, ni—ni kwa sababu ninakuja hapa kutengeneza hizi kanda. Hiyo ni ku... Sasa, zina... Mnaona, unaweza kuona mle chumbani ka—kanda ambazo zina—zinatengenezwa. Sasa... Na zinaenda kila pahali duniani kote.

²⁰ Sasa, hivi karibuni, Bwana akipenda, kuja huku, punde tu niondokapo hapa... Nitaondoka, Bwana akipenda, kesho asubuhi wakati fulani nirudi Arizona, kwa sababu nina mkutano uliopangwa huko. Halafu ni kuenda mpaka Kusini. Na ninyi watu wa Kusini kutoka kule Georgia, na Mississippi, na Texas, na Alabama, tunakuja mpaka kule chini, mpaka Florida moja kwa moja.

²¹ Ninaenda kutoka hapa mpaka Phoenix, halafu mpaka California, tena nirudi mpaka Dallas, na—na pengine niteremke mpaka San Antonio, nafikiri ni hiyo, tena nirudi kule Alabama, na Florida, na kupitia kule. Kwa hivyo tutawaoneni enyi watu kule chini, Bwana akipenda, moja kwa moja.

²² Na ndipo, nyinyi endeleeni kutuombea, na tutawajulisha wakati... Kama sisi—Bwana akituongoza tufanye—siku chache hapa haya majira ya kiangazi yajayo...

²³ Nilikuwa na mikutano kadha iliopangwa... Na wengi wenu kule New York mnajua wakati lile ono lilipokuja lililosema kwamba ile mikutano katika nchi ya Skandinevia... Mnaikumbuka ikitayarishwa kule? Na ndipo, nilipokuwa New York ono likaja kwamba kila mmoja wa ile mikutano

ingefutiliwa mbali kwa sababu fulani. Na ninakumbuka niliwaambia baadhi yenu mlilo hapa tulipokuwa kule New York. Na hivyo hasa ndivyo ilivyotendeka, kwa sababu wote walitaka siku moja na wasingepata lile jumba. Ndipo basi, hiyo yaweza kuacha nafasi ndogo kule mwezi wa Juni, huenda yakawa mapenzi ya Bwana, nilikuwa nikiwaza, pengine, kurudi kwa ajili ya zile Baragamu papa hapa kabla haijachelewa zaidi. Mnaona? Kwa hivyo twajua kuwa kila kitu hutendeka sawa kabisa. Bali hilo lilikuwa niani mwangu, basi huenda ikawa ndivyo anavyotaka tufanye.

²⁴ Sasa, naona mnabadilishana viti na—na nje ukumbini na kadhalika. Tungependa tungelikuwa na nafasi ya kuketi. Na sasa, tutakapozipata zile Baragumu, yaani—tunataka tupate lile jumba la michezo la shule ya sekondari—nafikiri linaweza kuketi watu elfu tano na mia tano na ndipo tutakuwa na nafasi ku—kila mtu awe na kiti na asikilize kwa utulivu tunapo—tunapohubiri, au... Zile—zile Baragumu, hizo ni nzuri sana, sana. Mimi... Katika kuzitazama juzi...

²⁵ Mnaona, katika ule Muhuri wa Sita, Baragamu zote Saba zinatoa sauti pale katika ule Muhuri wa Sita (mwaona?), kabla tu ule Muhuri wa Saba kufungua kuja kwa Kristo.

²⁶ Na usiku huu nina ujumbe muhimu sana ambao ningependa kuunena kabla tu ya ile—ile—ibada ya uponyaji. Na kama uko hapa na utakaa huku, vema, tutajaribu, kama itawezekana kuanza mapema kidogo, kwa sababu kutakuwa na mstari wa maombi. Sitahubiri muda mrefu sasa, lakini kuna kitu ambacho nilitaka kuliambia kanisa kwa muda fulani na kuwajulisheni juu ya—ya—ya—ya—jinsi mambo yanavyoendelea wakati huu na pale tu tunaposimama, na—nijuavyo mimi katika Maandiko.

²⁷ Sasa ningependa mfungue pamoja nami asubuhi hii—kama mngependa kuweka alama au kuandika mahali tunaposoma—Kitabu cha Isaya, na ningependa kusoma kutoka Isaya, sura ya 42 ya Isaya.

²⁸ Tunafurahi asubuhi hii pia kuwa na Ndugu Dauch akiketi pamoja nasi hapa. Mnapofungua... Mwajua, walidhani hataishi hapa Shreveport juzi, na hakika anayo imani...?... Naam, bwana! Anapanda moja kwa moja kutoka hali hiyo; Bwana ambariki yeye. Si... Mnaona, Ndugu Dauch ana miaka tisini na mmoja na alishikwa kabisa na ugonjwa wa moyo na hali kadhalika moyo kukoma kudunda. Na daktari yule yule aliyesema hayo alisema kwamba hakuona kwamba kuna njia yo yote ya yeye kuishi. Ndugu Dauch yu hai, na yule daktari amekufa. Mnaona, tu... Ndugu Dauch anaketi hapa.

²⁹ Na ndipo m—mtu mwenye umri wa miaka tisini na mmoja aliye na ugonjwa wa moyo pamoja na moyo kukoma kudunda. Na hapa nilipokuwa nikienda huko juu, nilimwona yuaja akitembea barabarani; nilimwona kanisani. Na nikaenda nikamwambia

akiwa katika hema la hewa ya oksijeni, “Katika Jina la Bwana, nitakusalimu kwa mkono katika . . . Nitakuona kanisani tena na kukusalimu kwa mkono barabarani.” Ile ibada iliyofuata tu, alikuwa hapa, akiketi papa hapa nyuma kanisani. Na nikaenda mpaka Louisville—tunapokula katika Blue Boar kule—kula, na mara nilipokuwa ninatoka katika gari langu, nikaanza kuenda juu barabarani, hapa yuaja Ndugu Dauch anateremka barabarani. Ilikuwa pale, kikamilifu kabisa. Na jinsi Bwana amembariki.

³⁰ Sasa, tutazungumza juu ya uponyaji usiku wa leo na mengineyo. Wana mambo maalum mno ya kuwaambieni usiku wa leo.

³¹ Bali, sasa, ili nipate zile kanda sasa, nao waweze kujitayarisha kuzianzisha, ningependa kuanza kusoma kutoka Isaya sura ya 42 na kifungu cha 1 hadi 7, na Mathayo sura ya 4, kuanzia, naamini, kifungu cha 15 na 16.

³² Sasa, katika—katika sura ya 42 ya—ya Isaya tutasoma.

Tazama mtumishi wangu nimegomezaye, mteule wangu, ambaye nafsi yangu imependezwa naye; nimetia roho yangu juu yake; naye atawatolea mataifa hukumu.

Hatalia, wala hatapaza sauti yake, wala kuifanya isikiwe katika njia kuu.

Mwanzi uliopondeka hatauvunja, wala utambi utokao moshi hatauzima; atatokeza hukumu kwa kweli.

Hatazimia, wala hatakata tamaa, hata ame—atakapoweka hukumu duniani; na visiwa vitazingojea sheria Zake.

BWANA . . . anena hivi, yeye aliyeziumba mbingu, na kuzitanda; yeye aliyeitandaza nchi na mazao yake; yeye awapaye pumzi watu walio juu yake, yeye awapaye roho wao waendao ndani yake.

Mimi, BWANA, nimekuita katika haki, nami nitakushika mkono, na kukulinda, na kukutoa uwe agano la watu, na nuru ya Mataifa;

Kuyafunua macho yaliyopofushwa, kuwatoa gerezeni waliofungwa, kuwatoa wale walioketi gizani katika nyumba ya kufungwa.

³³ Sasa, katika Injili ya Mathayo sura ya 4 ningependa kusoma kutimilika kwa ule unabii uliotolewa na Isaya. Katika sura ya 4 ya Mathayo ni—nitaanzia kusoma. Ikiwezekana hebuni tuanzie kifungu cha 12 badala ya cha 15.

Basi Yesu aliposikia ya kwamba Yohana amefungwa, alikwenda zake mpaka Galilaya;

. . . akatoka Nazareti, akaja akakaa Kapernaumu, mji ulio pwani, mipakani mwa Zabuloni na Naftali:

Ili litimie neno lililonenwa na nabii Isaya akisema,

Tazama—Nchi ya Zabuloni na nchi ya Naftali, Njia ya bahari, ng'ambo ya Yordani, Galilaya ya Mataifa,

Watu... waliokaa katika giza wameona mwanga mkuu, nao waliokaa katika nchi ya vivuli vya mauti mwanga umewazukia.

Tokea wakati huo Yesu alianza kuhubiri, na kusema, Tubuni; kwa maana ufalme wa mbinguni umekaribia.

Bwana na aongeze baraka Zake kwa kusomwa kwa Neno Lake.

³⁴ Na sasa, somo dogo la ajabu ambalo... Nilisikia mtu fulani akisema hivi, bali ningependa kuchukua hili liwe somo: *Yupo Mtu Hapa Anayeweza Kuiwasha Taa.*

³⁵ Na sasa, tutazungumza juu ya somo la Nuru. Hili linafuata masomo matatu ambayo tumekuwa tukizungumza juu yake, moja yake kule Tucson au Phoenix, juu ya mbona Yesu akapitia njia ya Bethlehemu. Hiyo... Lazima awe, kwa sababu Yeye ni *Bethlehemu. Bethlehemu, B-e-t-h* ni “nyumba”; *e-l*, “Mungu”; *e-h-a-m* ni “mkate, mkate—Nyumba ya Mkate wa Mungu.” Na kila Mkristo aliyezaliwa katika Kristo amezaliwa katika Bethlehemu, nyumba ya mkate wa Mungu.

³⁶ Ndiposa mle ndani ni—mfano wa Daudi aliyekuwa mtoro wakati wa kutengwa kwake na watu wake, alifukuzwa, na Bethlehemu ilikuwa imezingirwa, na Wafilisti waliizingira Bethlehemu. Na Daudi, mtoro, mfano wa kanisa leo—wa Kristo. Mnaona, Kristo ni mtoro kwa kanisa Lake leo. Wana... *Mtoro* ni “kitu kilichokataliwa.” Na Daudi alikuwa amekataliwa, ingawa alitiwa mafuta awe mfalme, lakini—nabii alikuwa amementia mafuta.

³⁷ Na katika wakati huu, akiwa m—mtoro kutoka kwa watu wake, alikuwa amejichagulia watu wengi hodari wa mataifa Mmoja wao aliva watu mia nane siku moja kwa mkuki—au upanga. Na mwingine aliruka shimoni na kumuua simba siku ya theluji. Na—na walikuwa wakikusanya dengu—ambazo ni maharagwe au mbaazi au kitu fulani—na—na hao wote wakatoroka, naye akasimama na kuua watu mpaka mkono wake ukachoka. Pia waliwaua wale majitu nduguze Goliathi. Wanaume shujaa, wakimshikilia Daudi, kwa sababu walijua yuaja mamlakani. Walijua hata yeyote aseme nini, Mungu alikuwa amementia Daudi mafuta, na walijua hivyo. Walikuwa wa Mataifa. Si hoja walimfukuza kiasi gani, walijua anakuja mamlakani. Na siku moja pale... .

³⁸ Ni mfano jinsi gani leo wa—wa Kristo, Mtoro? Unasema, “Kristo Mtoro?” Kulingana na Biblia ambayo tuna—Mungu ametupisha kwa uhodari katika hizo Nyakati Saba za Kanisa—hili kanisa la Laodikia, Kristo alikuwa mtoro nje ya kanisa Lake,

amekataliwa, akijaribu kurudi ndani tena. Yeye ni Mtoro wa kanisa Lake binafsi. Na sababu ya kuwa Mtoro ni kwa sababu Yeye ni Neno, na hawataliruhusu Neno liingie—wamepokea kanuni za imani badala yake.

³⁹ Na ndipo tunatambua basi, kwamba katika kule kushindana kukuu wale wanaume shujaa waliomzunguka—waliomzunguka Daudi, Mataifa . . .

⁴⁰ Kama mkichunguza jinsi Bethlehemu ilivyotengenezwa? Sitaki kuingia katika somo hilo. Lakini jinsi Bethlehemu . . . Hakika, Rahabu, yule kahaba, mwanawe ndiye aliyeanzisha Bethlehemu. Kilikuwa kituo cha ngano, na maji safi mengi pale. Naye akauanzisha ule mji mdogo. Na ulikuwa mdogo kabisa miongoni mwa miji yote, kwa maana nabii alisema, “Kutoka . . . Bethlehemu ya Uyahudi, hu mdogo kamwe katika majumbe ya miji ya Yerusalemu—au ya Uyahudi, bali kutoka kwako atatoka Mtawala atakayewatawala watu Wangu.” Kutoka ule ulio mdogo.

⁴¹ Daudi, alipochaguliwa pale juu, wale nduguze wakubwa na wazuri, wakati nabii Samweli alipanda kwenda kumtia mafuta, wote walikuwa wamesimama pale, wanaume wakuu shujaa, walionekana kana kwamba wangukuwa—kuonekana—walionekana wafalme wazuri, bali yule aliyakataliwa, Daudi, yeye ndiye aliyemwagiwa mafuta. Mji uliokataliwa ndio ambao Kristo . . . Waliokataliwa ndio ambao Kristo huwachukua (mnaona?), wale waliokataliwa.

⁴² Ndipo tunaona baada yake akaja Obedi, na baada yake akaja Boazi, na pale akaingia Mtaifa mwingine—ambaye aliingia kwa njia ya Ruthu—na kutoka pale akaja Yese, na kutoka kwa Yese akaja Daudi. Na zizi dogo kando ya kilima pale nje likamtoa Mfalme wa Wafalme, Yesu Kristo, Mwana wa Daudi, Mwanawe wa Kiroho.

⁴³ Sasa, ndipo alikuwa . . . Daudi mwenyewe akizaliwa mjini, Yeye ilimbidi aje hapa pahali padogo. Na paliitwa *Bethlehemu* ambayo maana yake ni “ile—ile nyumba ya Mkate wa Mungu.” Na Yeye ni Nyumba ya Mkate wa Mungu.

⁴⁴ Naye Daudi, akilala pale kilimani siku ile, na akatazama chini na kuona Wafilisti wamewazingira hivyo, lazima alijisikia mwenye joto na kiu. Akasema, “Lo laiti ningepata kinywaji kutoka kile kisima mara moja tena.” Kwani, wazo lake lililo dogo kabisa lilikuwa amri kwa—hao waliompenda.

⁴⁵ Ndivyo ilivyo leo, wazo lililo dogo sana la mawazo ya Yesu—au vipi kuhusu Neno Lake—lapaswa liwe amri kwetu watu wa Mataifa tumpendao. Kwani tunajua yuaja mamlakani hata akataliwe kiasi gani. Mbingu na nchi zitapita, bali hili bado litatawala vile vile wakati mbingu zote na nchi zote zimeondoka. Na tunajua Yeye yuaja mamlakani, kwani hakuna litazuia hilo kutendeka. Huyu ni Kristo, ufunuo Wake, na hili litatendeka

vile tu Neno linasema litatendeka, kwani Yeye ni Neno. Na amri Yake iliyo dogo sana ni... Hata iwe ndogo kiasi gani... Kama ni kubatizwa tena au iwe nini, tutalifanya kwa vyo vyote vile. Ni amri Yake.

⁴⁶ Na wazo la Daudi lililokuwa dogo sana lilikuwa amri kwa hao watu wa Mataifa, kwa sababu wao—mfano wa kanisa la Mataifa leo, wanaume shujaa. Waona? Wale wanaume waliosimama pamoja na Daudi walikuwa wa Mataifa, bali wanaume shujaa. Hawakuwa waoga. Hawakujua woga ulikuwa ni nini.

⁴⁷ Mwanamme mmoja alichukua upanga na kuwaua wanaume mia nane, wote wakimzunguka. Huyu alikuwa mwanamme wa namna gani. Mmoja wao, mmoja... Mmoja wa hao wanaume... Palikuwa na askari Mmisri aliyekimbia na mkuki mrefu; naye alikuwa na fimbo peke yake mkononi mwake. Akaichukua ile fimbo na kuugonga ule mkuki kutoka kwa mkono wake, akauchukua ule mkuki na kumuua mwenyewe. Mwaona?

⁴⁸ Mmoja wa wale majitu alikuwa na vidole inchi kumi na nne namna hiyo. Sasa, inchi kumi na nne... Kidole chako kina urefu sawa na mkono wako uliokunjwa. Ufungue huo; huo ungekuwa mkono wa nchi ishirini na nane. Na ana mkuki... Na akaruka mle ndani na kumuua. Mnaona? Kwa nini? Alikuwa mwanamme shujaa, mtu wa Mataifa akimtaazama mpakwa mafuta aliyejua yuaja jama lakani.

⁴⁹ Je, mlitambua, wao walikuwa mashujaa sana kwa Daudi, wakati Daudi hatimaye alikuja mamlakani, aliwafanya watawala juu ya miji. Je, si Yesu aliahidi yale yale? Jambo lile lile, kuwafanya watawala.

⁵⁰ Ndipo mle ndani, wakati shauku la Daudi lilikuwa kupata kinywaji safi... Pengine alikuwa na maji ya zamani, yenye joto, yaliyoharibika juu pale aliyokuwa anayanywa. Bali ikawa akafikiria yale maji safi pale chini katika Bethlehemu, “nyumba ya mkate wa Mungu.” Naye akasema, “Laiti ningepata kinywaji kutoka kile kisima...” Na wale wanaume wakazitoa panga zao na kupigana na Wafilisti maili kumi na tano, si kwa sababu aliwaomba wafanye hivyo, bali kwa sababu walijua aliyataka. Na wakawakata-kata wale Wafilisti mpaka wakafika kisimani. Wawili wao walipokuwa wakipigana mwingine alipata—ndoo yake ya maji na wakapigana tena wakirudi, safari yote ya kurudi, na kumpatia maji Daudi. Neno kuhusu ushujaa!

⁵¹ Daudi, yule mtu mcha Mungu, akasema, “Hasha! nisingeyanywa kutoka kwa hawa marafiki waliohatarisha maisha yao.” Naye akafanya toleo la kinywaji, akayamwaga ardhini kwa Bwana: “Mpeni Bwana. Ni yeye anayestahili hayo, si mimi.” Waliweka...

⁵² Mfano kamili wa Kristo Mwenyewe na Uzima Wake Mwenyewe wa Milele ndani Yake, lakini Mwamba uliopigwa,

akamwaga Uzima Wake ardhini kama toleo la dhambi kwa ajili yetu, ili Neno hili lipate kuishi.

⁵³ Lo, Mataifa, kama nilivyosema, ni nani atakayeufuta upanga ule pamoja nami? Yeye anataka kinywaji safi asubuhi hii, sio hizi kanuni bovu za kale za imani za makanisa na kadhalika tunazojipumbaza kwazo, Yeye anataka imani ya kweli katika Neno Lake watakaoamini kila Neno Lake. Na tuende kisimani na turudi na kinywaji, kiburudisho, ibada ambayo imejengwa, si juu ya kanuni za imani na dhehebu, bali ibada halisi ya Roho pamoja na Kristo miongoni mwetu akiishi Maisha Yake ndani yetu vile apendavyo kati yetu. Hiyo ni—hiyo si pamoja na kanuni za imani na mambo mbalimbali, hebu na tu—tuwe naye hivyo tu.

⁵⁴ Sasa, lifuatalo ni jinsi Mungu alivyotenda na wale watu kupitia ndoto katika siku za—za Yusufu. Je, ulitambua, ndoto ni za upili; ni njia ya upili ya Mungu ya kutenda jambo. Watu fulani wanaweza kuota ndoto, hazina maana yo yote. Unaweza kula zaidi kisha upate jinamizi. Ndoto ni njia ya upili. Waona? Vema, mbona Mungu amlinde Mwanawe kupitia njia ya upili? Alimtokea Yusufu. Kwa ulinzi wa mwanawe alioupeleka kwa njia ya upili. Je, umeshalifikiria hilo? Sababu hapakuwa na nabii nchini. Ilimbidi kutenda kupitia ndoto. Na haikuwa ndoto iliyohitaji kufasiriwa. Yule Malaika wa Bwana alisema, “Yusufu, usihofu kumchukua Mariamu mkeo, maana mimba yake ni kwa uwezo wa Roho Mtakatifu.”

⁵⁵ Lilikuwa jambo lisilokuwa la kawaida kwa hayo kutendeka. Yusufu akiwa mtu wa haki... Yeye—Yeye alikuwa asiye wa kawaida; Mungu si wa kawaida. Na lisilo la kawaida ni vigumu kulielewa. Hiyo ndiyo sababu ni vigumu kuelewa Kweli leo; ni jambo lisilo la kawaida sana. Mwanamke kumpata mtoto bila kumjua mwanamume, hilo lilikuwa lisilo la kawaida sana. Bali ukiwa mwaminifu na mnyofu, Mungu anaweza kukutokea katika ndoto. Hii yaonyesha kwamba lolote ulilo nalo, liwe niani mwako, iwe utapiga mbinja, uimbe, ushuhudie, au lolote ulifanyalo, kama utu wako wote umeumkabidhi Mungu, Mungu anaweza kuutumia ikiwa tu utamruhusu afanye hivyo.

⁵⁶ Halafu usiku uliofuata hapa Ndugu Neville akahubiri juu ya funzo la kuepuka, jinsi m—mtu anavyoepuka. Na nikafikiri kwamba ilikuwa ya kiajabu, na asubuhi hii Roho Mtakatifu yaonekana ananifanya ninene juu ya funzo la Nuru, jambo linalofuatia hasa. Kuenda kabisa mpaka mwanzo jinsi Maisha ya Kristo yalianzia horini. Tunatembea kurudi nyuma kabisa kuyapitia katika funzo letu. Na yeye hakujua, nami sikujua; na hapa lipo katika jambo lile lile. Mnaona? Kuendelea tu, linalofuata ni pale anapoingia katika huduma Yake. Na usiku wa leo tuna jambo ambalo litaambatana kabisa na hilo, kuendelea mbele kabisa usiku wa leo, Bwana akipenda.

⁵⁷ Sasa, Nuru kuu, watu wa Mataifa waliokaa katika sehemu za uvuli wa mauti, Nuru kuu ilizuka miongoni Mwao. Na Zabuloni, Naftali katika—njia ya Galilaya ya Mataifa, Nuru kuu—waliona Nuru kuu.

⁵⁸ Sasa nuru, mara ya kwanza nuru, tunaipata katika Biblia, inapatikana katika Mwanzo 1:3. Lilikuwa neno la Mungu lililolenwa likafanyika ile nuru. Mungu alisema, “Iwe nuru!” —Mwanzo 1:3—na ikawa nuru.

⁵⁹ Sasa kumbuka, basi nuru huja kwa neno lililolenwa la Mungu. Na nuru ndilo thibitisho, au jambo ambalo amelinena ni nuru. Nuru irukapo, yaonyesha kuwa... Mungu alisema, “Iwe nuru!” Hapakuweko nuru, na Yeye akasema, “Iwe nuru!” na ikawa nuru. Hilo ni thibitisho; nuru ni thibitisho la neno Lake lililolenwa. Jambo hilo hilo leo; thibitisho la neno Lake lililolenwa.

⁶⁰ Sasa, uonapo Neno Lake likithibitishwa, au kwa maneno mengine, likifanywa lilulikane, likihakikishwa, hiyo ni—ile Nuru ya neno Lake lililolenwa. Na bila nuru hakuna kinachoweza kuishi, bila nuru. Hakuna uzima duniani leo ambao—ila ule utakaokuja kutokana na—ile nuru ya jua, katika—katika Uhai wa mimea na kadhalika. Na hakuna Uzima wa Milele nje ya Mwana wa Mungu. Mnaona? Yeye ndiye ile Nuru.

⁶¹ Sasa, tunaona, naamini, tunapojifunza sasa... Na hii nuru... Nchi ilikuwa ukiwa.

⁶² Sasa, watu wengine hubishana mashuleni mwao na kadhalika jinsi dunia ilivyo na mamilioni ya miaka, na wakajaribu kulaumu Biblia, na kusema si sahihi, ni kwamba hawaisomi Biblia; hivyo tu. Kwa sababu Biblia haituambii umri wa dunia; Biblia ilisema, “Hapo mwanzo Mungu aliziumba mbingu na nchi. (Kikomo!)” Lini, aje, hivyo ni—hatujui hilo. Sasa, hiyo ni ya kwanza, na hicho ni “kikomo”; huo ni mwisho wa hilo fungu la maneno.

⁶³ “Hapo mwanzo Mungu aliziumba mbingu na nchi?” Pengine ilikuwa milioni mia moja au bilioni elfu moja, au chochote kile. Na jinsi alivyofanya, hiyo ni juu Yake kujua (waona?) si mimi. Bali dunia ilikuwa, nchi ilikuwa ukiwa, tena utupu, na maji yalikuwa juu ya—ya nchi; na Mungu akasema—ikaenda juu ya maji na akasema, “Iwe nuru!”

⁶⁴ Sasa, naamini kuwa jua na kadhalika tayari vilikuwepo. Naamini mwezi, unavyoendelea, Mwanzo 3, kueleza... Bali naamini kilichokuwa hapa... Kuwa dunia; tulikuwa tuitumie, na kwa hivyo... Na ikaingia; kulikuwa na ukungu na umande juu ya uso wa nchi, vikiitia giza. Kisha Mungu akasema, “Iwe Nuru!” na giza likatoweka, na kukawa na anga lisilo na mawingu.

⁶⁵ Na ninaamini hiyo ndiyo njia ya Mungu ya kufanya mambo; Yeye katika Biblia, kifungu kinachofuata—kifungu cha 4—

kinasema, “Naye akatenga nuru na giza, na nuru akaiita mchana, na giza akaliita usiku.” Na Neno la Mungu daima hutenga nuru na giza. Mnaona? Neno ndilo linalotenganisha (waona?), nuru kutoka kwa giza.

⁶⁶ Mungu daima hufanya jambo lile lile. Anapojitayarisha kutumia cho chote, kama alivyojitayarisha kutumia hii nyota ya kale—sijui ilikuwa nini, dunia hii—ilimbidi atenganishe nuru na giza. Anapojitayarisha ku—kutumia ki—kundi la watu, Yeye hutenganisha nuru na giza. Anapokuwa tayari kumtumia mtu binafsi, Yeye hutenganisha nuru na giza. Mnaona?

⁶⁷ Nuru huletwa na Mungu, na ile . . . Kumbuka, nuru ililetwa na Neno Lake lilolonenwa. Neno la Mungu lilisema, “Iwe nuru!” wakati hapakuwa na nuru. Na akaleta nuru itenganishe giza na nuru.

⁶⁸ Hili neno la amri lilisafisha anga kusudi jua lipate kuangaza. Na Neno Lake leo ndilo linalosafisha hali zote za kutokuamini.

⁶⁹ Nilikuwa nikizungumza . . . Nilikuwa na—nilikuwa na, nadhani mahojiano kumi na moja kabla tu ya kuja mimbarani asubuhi hii mle ndani. Baya sana . . .

⁷⁰ Juzi maskini rafiki yangu, Jim Poole, mvulana wake mdogo, walidhani alikuwa na ugonjwa wa moyo, wakamkimbiza hospitalini. Ilikuwa ugonjwa wa pumu, ukamtupa yule mvulana mdogo . . . Hangeweza . . . Moyo wake mdogo ukiruka, na kupumua, na—na anapiga mayowe na hangeweza kupata pumzi yake, na yule kijana mdogo akaonekana kama unakufa. Alipomfikisha hapa . . . Nami nilikuwa nikijitayarisha kuenda hospitalini; wakamleta hapa. Na nikaushika mkono wake mdogo, nikasema, “Nini kilichosababisha haya, ugonjwa wa surua umemkumba mtoto. Na ile surua, ile homa imemkumba kijana mdogo. Mtazameni, baada ya siku kadha nataka nimuone tena. Atakuwa amejaa surua.” Na hapa yupo amejaa surua. Mwaona, mwaona?

⁷¹ Sasa, nini . . . Mungu hutenganisha giza na nuru—au nuru na giza, na Yeye hutenganisha mauti na Uzima, na Yeye hufanya hivyo kwa Neno Lake. Neno Lake ndilo husababisha mambo haya daima.

⁷² Sasa, nuru ilikuwa . . . Sasa, ile mbegu tayari ilikuwa juu ya nchi. Naamini Mungu alikuwa amepanda mbegu, na mradi tu jua lingeifikia ile mbegu, ikaanza kukua. Na hiyo ndiyo sababu ilichukua tu siku kadha kuzaa haya, kwa sababu mbegu tayari ilikuwa ardhini. Ilichohitaji tu ni nuru.

⁷³ Na hivyo ndivyo Mungu amefanya leo; mbegu Yake tayari iko hapa, Neno Lake. Inachohitaji tu ni nuru juu Yake, na Yeye ndiye hiyo Nuru, kwani Yeye ndiye Neno. Neno na nuru ni kitu kimoja. Uhai uliomo mle ndani ndio Nuru ya Neno (unaona?) ndio ule Uhai. Ile chembe ya uzima iko katika punje, na punje ndiyo—uhai ndio unajitokeza na kuleta uhai kutoka kwa ile punje. Hivyo

ndivyo Kristo katika Neno analifanya Neno litende lipaswayo kutenda. Sawasawa kama uhai uliomo katika punje ya ngano au chochote kile; unaifanya ngano ifanye yaipasayo kufanya, kwa sababu ndio uhai ulio ndani yake.

⁷⁴ Uhai wote... Basi uzima huja tu kutokana na Neno la Mungu lililodhihirishwa. Uzima huja tu kutokana na Neno la Mungu lililodhihirishwa. Mradi tu liko katika kile kitabu hivi, laweza kushukiwa, bali likiisha kudhihirishwa, ndipo waona matokeo ya yale lilinena yakidhihirishwa; ndipo hiyo ni Nuru juu ya lile—juu ya lile Neno. Unaona? Hiyo ndiyo huleta... Neno lilisema hivyo, na ndipo likitimia, huo ni Uzima katika Nuru. Nuru ikileta Uzima.

⁷⁵ Nuru huleta uzima. Panda ngano hapa nje, ita... Uiweke katika orofa ya chini, uifunike kabisa, na ita—haitazaa cho chote, kwa maana haiwezi; hamna nuru mle. Lakini mara tu nuru inapoliangazia, ndipo itazaa uzima kama ni mbegu iliyo na chembe ya uzima. Na ndivyo ilivyo katika Neno. Unaona, Neno ni Mungu, na nuru inapoliangazia, inailleta—Nuru inapoliangazia, inalihuisha Neno tena. Kila wakati daima umekuwa hivyo.

⁷⁶ Lo, jinsi tunavyoyadhamini mambo haya makuu, jinsi kwamba lile Neno linapodhihirishwa ndilo ile Nuru ya lile Neno lililonenwa. Unaona? Mungu alisema, “Iwe nuru.” Sasa, vipi kama Yeye angesema tu, na nuru isiye? Basi hatujui kama ni kweli au la. Hatujui kama ako sawa, hatujui kama Yeye ni Mungu au la, kwa maana Yeye alisema tu, “Iwe”, na haikuwa. Mnaona? Ndipo basi Mungu anenapo na tunaona iko, basi hiyo ndiyo Nuru iangazayo, Ukweli wa lile Neno. Unaona? Pale ipo Nuru na Uzima.

⁷⁷ Uhai wote wa kimaumbile hutokana na Neno Lake lililonenwa, na jua ni neno Lake lililonenwa. Alisema aliumba nuru kuu angani ya mchana na nuru dogo ya usiku. Umeona? Na uhai wote wa kimaumbile sharti utokane na neno lililonenwa la Mungu. Ua haliwezi kukua bila nuru ya neno lililonenwa la Mungu kuliangazia, kwa maana jua ni—j-u-a—ni neno lililonenwa la Mungu aliposema, “Iwe nuru!” Unaona? Ni uzima ulionenwa wa Mungu, na si hoja watu watajaribu kiasi gani ku—kusema hiki, kite au kingine, bado yadumu vivyo: sharti uwe na hilo jua. Basi uhai, wa kimaumbile, utaweza kutokana tu na neno lililonenwa la Mungu.

⁷⁸ Na Uzima wa Kiroho, Uzima wa Milele, utaweza kutokana tu na Neno lililonenwa la Uzima la Mungu. Uzima ulikuwa yule M-w-a-n-a wakati huu. Ndani Yake mna Nuru, na ndani Yake hamna giza; na Yeye ni Nuru iliyonenwa ya Mungu (hiyo ni sawa?), Neno lililonenwa la Mungu; kwa maana *Hapo mwanzo kulikuweco Neno, naye Neno alikuweco kwa Mungu, naye Neno alikuwa Mungu*. Na daima hilo ni Mungu. Unaona? Na

inachukua Nuru ya Mungu kuliangazia Neno ili ilihuishe. Haya ni yale aliyonena, sasa hebu na Nuru iangaze (Amina!)—hebu na Nuru iangaze. Na ile Nuru italileta kila Neno katika mahali pake sahihi na katika majira yake. Amina!

⁷⁹ La! Mwaona, ifikapo wakati, wakati mwingine ile punje ndogo hulala kama iliyokufa ardhini wakati wote wa ba—baridi, kama mbegu, ngano ya majira ya baridi, imepandwa ardhini. Bali wakati lile jua linapokuwa sawa tu, lo, lazima itaishi. Mnaona? Na haiwezi kuishi bila jua. Na Mungu amefanya ahadi kwa kila wakati na kila siku, na ile Nuru inapokuwa sawa na kuangazia hiyo, itazaa yale hasa ambayo Neno lilisema; kwa maana Yeye ndiye Nuru na Uzima.

⁸⁰ Neno la Mungu hutokana tu na Biblia. Biblia ya Mungu ndiyo—umbo lililopigwa chapa la Mwana wa Mungu, kwa sababu Biblia ilisema kuwa hiyo ni ufunuo wa Yesu Kristo. Ni Mungu akijifunua Mwenyewe kupitia Kristo, na Kristo ndiye Neno. Na yahitaji ile Nuru ya Mungu kuliangazia lile Neno ilidhihirishe, kuthibitisha kwamba Mungu angali ananena Uzima—Uzima wa Milele, ananena... Nuru ya asili huleta uzima. Uzima huja tu kwa njia ya Nuru, lile Neno likidhihirishwa—au kufanywa mwili... Wakati ambapo ahadi zote zinakuwa—katika Biblia—zilipodhihirishwa ndipo Yesu Kristo, lile Neno, alifanywa mwili kati yetu. Mungu daima hufanya kazi kwa njia ya watu. Watu ni vyombo vya Mungu.

⁸¹ Sasa, ikiwa kutakuwa na joto kwenu hapa ndani, mwaweza kuteremsha madirisha au lolote mpendalo, mzime tanuru, labda ba—bawabu anaweza kuupunguza ule moto wa tanuru kidogo. Naona wengi wanaona joto, na ni joto kusimama hapa pia. Basi—basi kumbuka kwamba... Ninafurahi kuna joto badala ya baridi, kwa sababu ni—ninapenda joto, ni... Joto daima huleta nuru—uzima. Yahitaji moto...

⁸² Angalieni! Sasa, kufanywa mwili, Neno linapofanyika mwili, hudhihirishwa. Kwa mfano lichukue Neno na uliweke katika mahali pake sahihi, ardhi ya aina nzuri, litazaa—ile—ile mbegu itazaa kwa jinsi yake. Nalo Neno likiletwa katika moyo wa aina sawa, litajidhihirisha lenyewe. Litaleta nuru. Itajitokeza juu yake. Sawa.

⁸³ Hakuna cha asili—hakuna cha asili wala cha kiroho kiwezacho kuishi bila Nuru ya Mungu. Uzima basi waweza kuja tu kwa njia ya Nuru. Hakuna cha asili wala cha kiroho kiwezacho kuishi bila Nuru ya Mungu. Fikiria hilo. Sawa. Bali atutumiapo ile Nuru (mnaona?) na kufanya mambo haya yote, halafu tuikatae... Sasa, hiyo ndiyo sehemu ya kusikitisha ni wakati Nuru inakataliwa wakati imetumwa kwetu.

⁸⁴ Sasa, ungemfikiria mtu leo akisema, “Ninakataa kabisa kusema kwamba kuna kitu kama jua. Siamini kuna jua.” Na anakimbilia orofa ya chini, na—na anafunga milango yote, na

kuketi nyuma kwenye giza, na kusema, “Hakuna kitu kama jua; hakuna kitu kama nuru.” Ungejua papo hapo kwamba bongo za mtu huyo zina kasoro. Waona? Ana kasoro anaporudi mbio katika orofa ya chini kwenye giza na kukataa kukubali faida ya nuru inayotolewa na Mungu. Mtu huyo ana kasoro. Hataki mwali wake wenye joto. Hataki nguvu zake ziletazo afya. Hataki nuru yake atembe ndani yake; ni heri yeye akae gizani. Yaonyesha bongoni kuna kasoro, kwa kawaida, kwa huyo mtu.

⁸⁵ Na ninasema hili kwa upendo wote pamoja na heshima: Vivyo hivyo basi kuna kasoro kiroho kwa mtu atakayerudi mbio katika madhehebu yake yenye kanuni za imani na akatae kuona Nuru ya Biblia inapoangaza mbele yake. Mtu huyo ana kasoro! Anarudi katika kanuni zake na desturi na kufunga mlango, na kusema, “Hakuna kitu kama hicho. Siku za miujiza zimekwisha. Hakuna kitu kama uponyaji wa Kiungu. Hakuna lolote la mambo haya. Hayo yalikuwa kwa mtume.” Mtu huyo ana wazimu wa kiroho. Unaona? Ana kasoro. Yeye—yeye—yeye amefunga mapazia na—na kumkataa Roho Mtakatifu awezaye kumjilia. Kama Yeye anaweza. . . “Ninyi mkikaa ndani Yangu na Neno Langu liwe ndani yenu, ndipo (ile Nuru ikiangaza juu ya hili Neno) ombeni mtakalo.” Mnaona, mnaona?

⁸⁶ Kuna kasoro kwamba atakataa chemchemi tulizopewa na Mungu tuishi kwazo, Neno Lake. “Mwenye haki ataishi kwa imani. Na mtu hataishi kwa mkate tu, ila kwa kila Neno, si sehemu ya Neno, kila Neno litokalo katika kinywa cha Mungu.” Na mtu anapokataa tu hilo, ana kasoro, ujuzi wake una walakini ambapo anadai kuwa anampenda Mungu halafu amkatae Mungu. Mtu huyo ana walakini. Twajua hilo bila shaka lo lote. Analikataa, anakimbilia mahali hapa, na kusema, “Sasa, ni—tu—sitaki kujua lolote kulihusu; usiniambie lolote kuhusu mambo haya. Si—siamini lolote kulihusu. Wewe. . . Hata useme nini. . .”

⁸⁷ Mtu fulani alisema sio muda mrefu uliopita—nilikuwa ninawaambia kuhusu—alisema, “Sijali kama ungeleta wenye kansa hamsini na madaktari hamsini washuhudie, siamini. Sijali kama ungewafufua wafu papa hapa mbele yangu, singeamini.” Mnaona, mtu huyo ana kasoro. Kuna—kuna—kuna. . . Na hata hivyo huyo mtu alikuwa mhudumu (Unaona, unaona?)—anadhaniwa kuwa mhudumu. Lakini tu kwa vile lile dhehebu haliamini katika—katika uwezo wa Mungu, haliamini kuwa lile Neno lilimaanisha tu yale lilisema, huyo mtu anakimbilia hii orofa ya chini, iliyochakaa, chafu, orofa ya chini iliyo bovu ya dhehebu na kukataa joto na miali itoayo Uzima ya Roho Mtakatifu, Yesu Kristo, aliye yeye yule jana, leo, na hata milele. Basi mtu huyo ana kasoro. Mnaona? Laiti angaliishi katika ule ubaya, giza, na kadhalika badala ya kuishi katika Nuru ya Mungu na ya Biblia iliyosema kuwa Yesu Kristo ni yeye yule jana, leo, na hata milele. “Kazi nizifanyazo mimi, ninyi

nanyi mtazifanya; naam, na kubwa kuliko hizo mtafanya, kwa maana Mimi naenda kwa Baba.” Mtu huyo ana walakini. Bila swali lolote, kuna kasoro fulani.

⁸⁸ Na wewe mtu unayesikiliza haya mahali pengine duniani, popote ulipo, ujuzi wako una kasoro unaposema kwamba unampenda Mungu na kulikataa Neno Lake. Kuna kitu... Unakataa lile... Si ajabu yale mambo hayawezi—kanisa liko katika hali lilivyo na mambo hayawezi kutendeka vile Mungu aliahidi, ni kwa sababu hamtalipokea Neno wala kutembea katika ile Nuru. Biblia ilisema, “Na tutembea katika Nuru kama vile Yeye alivyo katika Nuru, ndipo Damu ya Yesu Kristo, Mwana wa Mungu, yatusafisha dhambi yote.” Dhambi ni kutokuamini.

⁸⁹ Basi ikiwa tunatembea katika Nuru iliyotolewa na Mungu ya wakati huu, ndipo Mungu analichukua lile Neno ambalo limetolewa kwa wakati huu na kulithibitisha kama alivyofanya katika Mwanzo 1:3. Alisema, “Iwe Nuru!” ikawa Nuru. Neno Lake lilitoka, na nuru ikalifuata na kuondoa ule ukungu. Na giza likaenda katika pembe moja, nayo nuru ikaangaza upande mwingine.

⁹⁰ Hivyo ndivyo Mungu afanyavyo leo. Analituma Neno Lake la saa hii, na Roho Mtakatifu anakuja na kulihuisha hilo Neno. Na giza linaingia katika kanuni zao na madhehebu yao, bali Nuru huangaza; kwa sababu ni Neno la Mungu likidhihirishwa kuwa Neno Lake ni kweli. Sasa, hakuna la kubuniwa katika hayo, hayo ni Maandiko kabisa. Sawa.

⁹¹ Sasa, tunaona kuwa wale—wale mamajusi, mamajusi wa zamani walifuata bayana iliyotolewa na Mungu; walilifuata Neno la Mungu mpaka kwa ile Nuru, kwa maana ni Neno lililoleta Uzima.

⁹² Sasa, wasema, “Walifuataje?” Naam, walikuwa mamajusi, twafahamu. Na ndipo tunaona kwa nabii Baalamu—kule nyuma katika Hesabu 24:17—Baalamu mwenyewe alikuwa aina ya mamajusi. Alikuwa nabii, kwa kweli, naye akatabiri hapa akasema nyota itatokea katika Yakobo. Na wakati hawa mamajusi walipoona ya kwamba Neno la Mungu lilisema nyota itatokea kwa Yakobo, waliifuata ile ishara ndogo iliyotolewa na Mungu mpaka chanzo cha Nuru ya milele. Ndivyo watakavyofanya mamajusi wa siku hizi ambao hawajapofushwa na kanuni za imani, watalifuata Neno lililotolewa na kunenwa na Mungu mpaka wauone ukamilifu wa uweza wa Mungu ukichanua katika saa hii. Mnaona? Wao—wao wanaliona, na wanajua kwamba hiyo iko hapa katika Maandiko. Mungu aliahidi kwa siku hii.

⁹³ Si hoja mahali pangapi pa kuangalilia nyota, au mambo mengine mangapi yaliwaambia wale mamajusi, “Naam, mmerukwa na akili!”... Miaka miwili walikuwa safarini. Waliyapita mataifa mengi, nao wakasema, “Mnaenda wapi?”

⁹⁴ “Lo, tuliiona nyota Yake mashariki nasi tumekuja kumsujudia.” Na walipojipanga kule Yerusalemu, makao makuu ya madhehebu, hawakuwa na jawabu. Walitembea huku na huko katika barabara za mji wakilia, “Yuko wapi Yeye aliyezaliwa Mfalme wa Wayahudi?” Hawakujua lolote kuhusu hilo. Basi wakaliendea Neno, wakatafute. Walikuwa wamefuata, walijua ile nyota ilikuwa ikiwaongoza kwenye Nuru ya milele. “Tuongoze hadi kwenye Nuru Yako kamilifu.” Na Neno ndilo likuongozalo kwenye ile Nuru, nayo Nuru ndiyo hulidhihirisha Neno.

⁹⁵ Angalia, walikuwa watu wenye hekima, na wenye hekima leo, sio hekima. . . Hekima ya ulimwengu huu ni upumbavu kwa Mungu. Wanasayansi wenu wote, na ninyi watu mnaotegemea elimu kuu fulani au jambo lingine likiwaambia namna ya kupasua atomi, haiwezi kuwapa Uzima. Hakuna liwezalo kuwapa Uzima isipokuwa Neno Lililonenwa la Mungu. Ndiyo njia pekee ambayo Uzima waweza kujia ni kupitia Neno Lake Lililonenwa.

⁹⁶ Hiyo ni sawa kujua namna ya kupasua atomi, ningapenda wasingalijua namna ya kufanya hivyo. Lakini kama wa. . . Lazima wafanye hayo, kwa sababu ulimwengu huu unaning’inia leo. . . Ilikuwa lazima itendeke kupasua haya mashimo makubwa ardhini kufanya hayo mawe yaliyoyeyuka yatoke na kufanya upya ulimwengu huu tena na kutengeneza nchi mpya, ambako wenye haki watatembea juu ya majivu ya waovu, ambapo dhambi itisahauliwa. Kila kitu kina njia ya kujifanya upya tena. Na mtu aliyejaliwa kuishi katika dunia hii kwa hekima yake—akiuchukua mti wa ujuzi badala ya mti wa uzima—ataiharibu dunia ambayo Mungu alimpa aishi juu yake. Bali wale ambao bado wako katika Mti wa Uzima watakuja katika mbingu mpya na nchi mpya ambapo hapana ugonjwa wala mauti. Nuru, Nuru! Bwana; tutumie Nuru.

⁹⁷ Ni Malaika wa Mungu walioangaza nuru juu ya kilima kuwaongoza wale wachungaji kwenye Nuru ya milele. Mnaona, huja tu kupitia kwa Nuru. Uzima unaweza tu kuja kwa njia ya Nuru. Wachungaji wakitaka kujua. . . Mnajua, wakati mfalme anapozaliwa, wao huimba, sherehe kuu mfalme anapozaliwa. Sasa, yeye alizaliwa kisiri sana na kuzaliwa zizini, katika—horini ambapo ng’ombe na farasi walikuwa wanakulia, lakini hata hivyo Yeye alikuwa Mfalme. Na wale—wale Malaika walishuka na kuimba nyimbo kwa wachungaji katika nuru. Wale Malaika wenyewe walikuwa nuru zilizoangaza na Neno la Mungu. . . Walikuwa na Neno la Mungu, na kuwaambia, “Leo katika mji wa Daudi, au katika Bethlehemu amezaliwa Kristo Mwokozi.” Malaika walikuwa na Neno, nalo Neno lilikuja kwa njia ya Nuru iliongoze. Nao wakalifuata Neno la wale Malaika mpaka Nuru ya milele. Wakampata mtoto pale amefungwa

katika nguo za kitoto kama walivyosema. Kwani waona, Uzima hutokana tu na Nuru.

⁹⁸ Angalia, Yeye alikuwa lile Neno likifanywa Nuru, au akawa Nuru. Lile Neno... Katika kile kizazi Yeye alikuwa Neno Nuru ya kizazi hicho, kwa sababu manabii wa kale walikuwa wamenena kumhusu Yeye, na hapa yuaja na kuthibitisha kuwa Yeye alikuwa Nuru ya Neno lililonenwa la Mungu. Unaona? Yote manabii waliyokuwa—walikuwa wamenena yalikuwa yametimizwa katika Yeye. Mnaona? Manabii hapa nyuma na lile Neno—kama Mungu alivyokuwa katika mwanzo aliposema, “Iwe nuru!” na nuru ikaja—sasa, nabii alisema, “Bikira atachukua mimba, atamzaa Mtoto Mwanamume. Watamwita Jina Lake Imanueli, kwa maana atakuwa Mungu pamoja nasi.” Sasa, walikuwa wamelinena; Neno lilikuwa limetoka, bali Yeye alikuwa ile Nuru. Yeye alikuwa nini? Ule utimilizo. Haleluya! Yeye alikuwa utimilizo wa lile Neno. Yeye alikuwa dhihirisho la hilo Neno.

⁹⁹ Ndivyo ilivyo leo. Neno la Mungu lilikuwa limetimizwa wakati ule; hiyo ndiyo Nuru. Ni Mungu akijidhihirisha Mwenyewe. Yeye alikuwa Nuru ya ulimwengu.

¹⁰⁰ Na wakati manabii kwa uongozi wa Roho Mtakatifu waliposema, “Kwa ajili yetu Mtoto amezaliwa; tumepeva M—Mtoto Mwanamume—au tumepeva Mtoto; naye ataitwa Jina Lake Mshauri, Mfalme wa Amani, Mungu Mwenye Nguvu, Baba wa Milele,” alikuwa pale. Alikuwa nini? Nuru iliyotimiza Neno hilo (Amina!), Nuru iliyotimiza Neno hilo.

¹⁰¹ Katika Mathayo—katika Mathayo Mt. sura ya 28 twaona, na Yesu alipofufuka kutoka kwa wafu, Yeye pia alikuwa Nuru ya Neno lililonenwa la Daudi lililosema, “Sitaiacha roho Yake katika kuzimu; wala sitamtoa Mtakatifu Wangu aone uharibifu.” Mauti yalikuwa katika giza, bali Yeye alizivunja muhuri za mauti, na kuingia ndani yake, na kutoka humo tena. Alikuwa ile Nuru, Neno lililothibitishwa kwamba wafu wanaweza kuishi baada ya mauti. Yeye alikuwa hivyo!

¹⁰² Siku ya Pentekoste hiyo ilikuwa ile Nuru iliyoangaza wakati Roho Mtakatifu alikuwa amekuja. Isaya lisema katika sura ya 28 ya Isaya, Isaya alisema pamoja na—amri lazima iwe juu ya amri; kanuni lazima iwe juu ya kanuni, huku kidogo na huku kidogo; lishikeni lililo jema; sababu kwa midomo ya watu wageni na kwa lugha nyingine nitasema na watu hawa; na hii ndiyo raha—hii ndiyo Sabato nitakayowapeni.” Katika haya yote hawangesikia, waliondoka na kutikisa vichwa vyao. Na ndipo katika siku ya Pentekoste wakati Roho Mtakatifu alipowajilia watu hao, na wakatenda kama wanaume na wanawake walevi, wakiyumbayumba kwa uweza wa Roho Mtakatifu, na wale—wakaondoka na kutikisa vichwa vyao, “Watu hawa wamelewa,

wamejawa na divai mpya,” na kadhalika. Hiyo ilikuwa ile Nuru hasa, lile Neno ambalo lilikuwa limetabiriwa likidhihirishwa.

¹⁰³ Ndivyo ilivyo katika kila wakati. Lile Neno likidhihirishwa, likihuishwa ndilo Nuru ya wakati huo, pale—lile Neno likidhihirishwa sawasawa na lilivyokuwa katika Mwanzo 1 wakati Mungu alisema, “Iwe nuru,” ikawa nuru, wakati Mungu alisema kutakuwa na Mtoto Mwanamume, na kukawa na Mtoto Mwanamume.

¹⁰⁴ Mungu aliposema katika Yoeli 2:28, “Hata itakuwa katika siku za mwisho nitaimwaga Roho Yangu juu ya wote wenye mwili. Wana wenu, waume kwa wake, watatabiri. Juu ya watumishi wangu, wanaume kwa wanawake, nitaimwaga Roho yangu. Vijana wenu wa kume wataona maono; wazee wenu wataota ndoto!” Na mambo haya yote aliyoahidi, wakati Huyo, Roho Mtakatifu aliposhuka, ilikuwa Nuru juu ya lile Neno. Wakati lile Neno lilipodhihirishwa, ndipo likawa Nuru. Yeye ndiye Nuru. Yeye ndiye Nuru itupasayo kuifuata. Yeye ndiye Nuru ya pekee. Malaika walipata nuru na wakaifuata mpaka wakamfikia Yeye.

¹⁰⁵ Sasa, katika nyakati zote Mungu ametenga kiasi fulani cha Neno Lake kwa kila wakati. Mungu daima humpeleka mtu fulani ambaye lile Neno laweza kuingia ndani yake na kuonyesha Nuru yake. Ili . . . Katika kila wakati inafanya jambo lile lile, daima hufanya hivyo.

¹⁰⁶ Yeye alikuwa timilizo, kama nilivyosema, la nguvu zote za Kiungu, nguvu takatifu za manabii. Walikuwa miungu wadogo. Wakati Neno la Bwana lilimjia mtu, Yesu Mwenyewe alisema kwamba huyo alikuwa mungu. Mwajua hayo. Alisema, “Kama sheria yenu ilisema, na baba zenu kule nyuma, iliwaita wale waliojiliwa na Neno la Mungu—iliwaita miungu, mwanilaumuje Mimi nikisema—niliposema Mimi ni Mwana wa Mungu huyo?” Mnaona? Wakati Mungu yule yule Mwenyewe aliyenena lile Neno kupitia manabii, Yeye alikuwa dhihirisho la lile Neno lililonenwa. Na kama nabii alitwa mungu kwa sababu alikuwa dhihirisho la Neno la nabii mwingine, kngemulaumje Yeye ambapo Yeye alikuwa jambo lile lile? Alikuwa Mwana wa Mungu. Kwa kuwa ataitwa Mwana wa Mungu.

¹⁰⁷ Yeye alikuwa Masihi aliyeahidiwa tangu zamani ambaye ulimwengu ulimngojea. Alikuwa ahadi ya Masihi ikidhihirishwa.

¹⁰⁸ Mtazame Yeye wakati alisimama pale. Alisema, “Kama sizitendi kazi za Baba Yangu, basi nilaumuni. (Mnaona?) Bali kama hamniamini Mimi, ziamini kazi nizatendazo. Zanishuhudia mimi ni Nani. Zawaambia Mimi ni Nani.” Mwaona ile saa ya upofu na yenye giza waliyoishi, hawangeiona. Hawangeweza kuelewa, jinsi Yeye angekuwa hayo. “Anawezaje kuwa mwana yeyote wa Mungu naye alizaliwa papa hapa

Bethlehemu?” Laiti wangejua, Neno lilisema kwamba Yeye angekuja hivyo.

“Mbona, baba yake Yusufu ni seremala. Mama yake, kwani, hata inaaminiwa miongoni mwa ndugu zetu kwamba alizaliwa haramu.” Mnaona? Lakini hata hivyo Neno la Mungu lilisema hivyo.

¹⁰⁹ Alisema, “Mwayachunguza Maandiko, kwa sababu mnadhani kwamba ninyi mna Uzima wa Milele ndani yake, na hayo ndiyo yanayonishuhudia Mimi ni Nani. Hayo ndiyo yanayonishuhudia,” hayo Maandiko Matakatifu. Basi Yeye alikuwa nini? Nuru ya Mungu. Si ajabu alisema, “Mimi ndimi Nuru ya ulimwengu.”

¹¹⁰ Hakusema tu, “Mimi ndimi Nuru,” bali alisema, “Ninyi ni Nuru.” Kama Neno Lake liko ndani yenu likijishuhudia Lenyewe, basi ninyi ni Nuru ya Ulimwengu.”

¹¹¹ Angalia, twatambua, Nuru ya kila wakati ikidhihirishwa tu sawa. Basi nataka kuuliza swali kama—kabla wakati wetu kwisha. Mbona, mbona basi wali—waliikataa? Wangeikataaje wakati ile—Biblia yao wenyewe waliyokuwa wakiisoma ilikuwa ikidhihirishwa mbele zao. Sasa, jifunzeni kwa bidii sasa.

¹¹² Sasa kumbuka, ninawazungumzia watu wengi wakati huu (mwaona?), sio tu yapata mia nne au tano walio hapa. Lakini ni—ninazungumzia elfu nyingi.

¹¹³ Tulieni tu kwa dakika moja. Simamisha mashine yako ya kucheza kanda na uulize swali: Mbona watu wa kidini, watu wazuri. . . Mbona Yusufu ashuku? Unaona? Mbona Yu. . .? Kwa sababu hakuyachunguza Maandiko. Mbona makuhani washuku? Sababu moja. . . Hawakuyachunguza; walijua. Nikodemu alisema sawa; alisema, “Rabi, twajua ya kuwa u mwalimu, umetoka kwa Mungu. Hakuna mtu awezaye kuzifanya ishara hizi uzifanyazo wewe, isipokuwa Mungu yu pamoja naye. Twajua hayo.” Lakini ilikuwa nini? Mapokeo yao yaliwazuia kufanya hivyo.

¹¹⁴ Basi mbona walikuwa—wakamkataa Masihi? Ni. . . Mbona waliikataa ile Nuru? Hapa kuna Neno walilolijua kwamba litatimia, bali lile Neno lilipodhihirishwa kuonyesha kwamba Neno la Mungu limetimia. . . Linganisha hilo na leo. Unaona? Wakati pale, imeandikwa katika Neno kwamba itatendeka. . . Basi mbona watu wale wakalikataa, waalimu? Kwa sababu walikuwa wanaishi katika mng’aro wa nuru nyingine. Ndivyo. Walikuwa wanaishi katika mng’aro. Hilo ndilo jambo wanalofanya leo. Wanaishi. . . Sababu ya kuikataa, ni kwa sababu wanaishi katika mng’aro wa nuru nyingine. Mnaona? Sasa, walikuwa wanaishi katika mng’aro wa yale Musa alisema—walidai. Walikuwa wakiishi katika mng’aro wa wakati mwingine uliopita. Na leo hiyo ndiyo sababu ile ile ambayo huu Ujumbe kwamba Yesu Kristo bado ni yeye yule unakataliwa, kwa sababu

watu wanaishi katika ming'aro ya nyakati zingine. Kwa sababu ile ile wanaikataa.

115 Sasa tunaona. Na Webster anasema kwamba *mng'aro* ni kitu “kama nuru bandia.” *Mng'aro* ni “nuru bandia,” kitu kile kile king'aracho. Kama—kama mazigazi barabarani, unaenda barabarani, wengi wenu mnaoendesha magari, na kuangalia chini mbele yako unapoliona jua chini, inarudisha nuru—na kama mazigazi—inaonekana kana kwamba kuna maji kote barabarani. Bali unapofika pale, hakuna kitu pale. Ni mazigazi tu ya uongo, *mng'aro* wa nuru ya kweli. Hayo ndiyo ibilisi anafanya leo, anawaonyesha watu mazigazi, Halmashauri ya Makanisa, kundi la madhehebu ambayo hatimaye yataonekana kuwa ni bandia. Sababu yake ni kwamba kuna Nuru ya kweli inaangaza. Kama ile Nuru ya kweli haingekuwa inaangaza yale mazigazi hayangekuwako. Nuru ya kweli huangaza. Katika hilo wanaishi katika *mng'ao* wa wakati mwingine, jambo lingine, kwa maana imegonga na ikapita.

116 Sasa, *mng'aro*, haya mazigazi ni ya bandia. Ni *mng'ao* wa jua. Na hivyo ndivyo, walifanya jambo lile lile. *Mng'ao* bandia wa Nuru ya kweli. . .

117 Sasa, ilithibitika kuwa Yeye alikuwa Nuru ya kweli. Alikuwa ile Nuru. Kwani walijua kuwa Yeye alikuwa ile Nuru? Ungejuaje kuwa Yeye alikuwa ile Nuru? Kwa sababu Neno lililoahidiwa lilidhihirishwa kupitia Kwake, kwa hivyo Yeye alikuwa ile Nuru ya lile Neno lililonenwa. Amina! Jamani, hilo karibu lingenifanya mimi Mbaptisti wa Kipentekoste nipige mayowe.

118 Angalia, fikiria hilo, *mng'aro*. Unaona. Kuishi katika *mng'aro*. Lakini wakati Neno la kweli linaishi, hiyo ndiyo Nuru, yale Mungu alisema. Sasa, vipi kama Mungu alisema pale Mwanzo, “Iwe nuru,” vema, na kitu kengine kijitokeze (mnaona?), ni mazigazi tu. Mnaona? Halingekuwa lile—yale Mungu alisema. La, halingekuwa. Vipi kama Mungu angelisema, “Iwe nuru,” na ukungu zaidi uje? Unaona? Haingekuwa nuru. Lakini sababu ya kuja kwa nuru, lilikuwa Neno Lake likidhihirishwa. Na leo Mungu asemapo mambo kama hayo yatatendeka wakati huu na unayaona yakitendeka, hiyo ni nini? Ni Nuru katika Neno la Mungu. Ni Neno likifanywa Nuru, likijidhihirisha Lenyewe.

119 Sasa, wao walisema, “Ninyi mwasema tu akina nani?” “Mbona,” alisema. . . “Mnajaribu ku. . . Tunajua kuwa una wazimu. Mbona, u Msamaria; huna akili timamu. Mbona, unajaribu ku. . . Nani awezaye kusema. . . Tunajua ulizaliwa katika dhambi. Hatujui unakotoka. Hakuna habari ya kitambulisho chako katika makundi yetu. Mbona, una wazimu. Una pepo mchafu.” Unaona? Kasema, “Naam, umerukwa na akili.” Lakini Yeye alikuwa ile Nuru ya Mungu halisi na ya kweli ikiangaza, na *mng'aro* ulikuwa umewapofusha macho yao.

“Tuna Musa kama kiongozi wetu.”

¹²⁰ Akasema, “Kama mngemwamini Musa, mngalinijua Mimi.” Na kama mngemwamini Yesu na Biblia, mngelijua saa hii mnayoishi.

¹²¹ Wanasema, “Vema, sisi ni Wakristo; sisi...” Kama mngekuwa hivyo, mngezijua kazi za Kristo kwa siku hii. Mnaona, mnaona? Mngezijua.

¹²² Yesu alisema, “Manabii hao wote walinena habari Zangu. Na kama mngewaamini wale manabii, hata, mngenijua Mimi. Kazi Zangu zanitambulisha, kwa sababu yale yalisemwa ningeyafanya, ninayafanya. Na ni nani awezaye kunihukumu sasa kwa kutokuamini?” Na bado hawakuliona. Kwa nini? Macho yao yalifungwa kwa mng’aro (mnaona?), mng’aro wa kitu kingine ambacho walichukua kuwa ndivyo Neno lililonenwa la kweli lilivyo. . .

¹²³ Sasa lifikirie! Lifikirie! Walidai kuwa wanaliamini hilo Neno. Lakini desturi zao ziligeuza nyuso zao kutoka kwa Neno la kweli na kuelekea mng’aro; basi, hawangeona jambo halisi. Ndivyo ilivyo leo. Ndivyo imekuwa katika kila wakati. Mnaona, Ne—Neno la kweli huangaza, bali wamezoea mapokeo sana hivi kwamba hawawezi kuona lile Neno. Wanauangalia mng’aro, nao ni vipofu. Mng’aro utakupofusha. Kuna kimeta toka kwake, kitakupofusha, na kitafanya. . . Wakati ile. . .

¹²⁴ Yesu alisema “Nyinyi ni vipofu wanaoongoza vipofu.” Walipaswa kuliona, kuona Yeye alikuwa ni Nani, bali hawakuweza kwa sababu walikuwa wanaishi katika mng’aro huo.

¹²⁵ Sasa, mng’aro, kama nilivyosema, ni nuru bandia, mazigazi, wazo bandia la Nuru ya kweli, wazo bandia. Ni kitu ambacho—ambacho kinapaswa kufanana nayo, bali sicho hicho.

¹²⁶ Sasa, njia pekee ya wao kutofautisha, kwa sababu yale mambo ambayo Yesu alifanya yalithibitisha Yeye alikuwa Nani, kwamba Yeye alikuwa ile Nuru. Wao walidhani kuwa walikuwa katika nuru. Bali sasa, kama ungetulia tu kidogo na kufikiria, ni nani aliye katika Nuru basi?

¹²⁷ Sasa leo, kama kosa la kufikiria kama hilo lilifanywa na watu wa makanisa wa siku ile, jambo la kufikiria hivyo lilifanywa, ndugu zanguni, hamfikiri kuwa wakati umewadia kwetu kutulia na kufikiria Nuru ni nini? Tusifanye kosa la kufikiria jinsi hiyo. Lakini mnafanya hivyo. Tayari mmefanya (mwaona?) na hamkujua. Sawa na vile ilivyokuwa wakati huo.

¹²⁸ Sasa, koma tu kwa dakika moja uone Neno lasema nini kwa siku hii. Kama wangekoma na kufikiri, “Ndiye huyu hapa anatimiza kikamilifu kabisa yale Neno lilisema atafanya,” . . . Na akawahimiza vile ninavyowahimizeni ninyi. Ninawahimiza ninyi kuangalia katika Neno, yachunguzeni Maandiko, muone

kama hii siyo ile saa. “Mwayachunguza Maandiko; mnadhani kwamba ninyi mna Uzima wa Milele ndani yake, na hayo ndiyo yanayonishuhudia.” Hayo ndiyo yanayoishuhudia kazi hii leo. Kazi yenyewe yashuhudia kwamba inafanywa. Na Maandiko yanasema kwamba itafanywa, basi ni Nuru ya saa hii. Neno la Mungu lilisema hivyo.

¹²⁹ Mapokeo yenu na kadhalika ni vile hasa Biblia ilisema, kama wale waliotikisa vichwa vyao na kuondoka. Meza zote zimejaa matapiko Biblia ilisema. Na hivyo ndivyo walivyo... Hawangeamini, walitikisa vichwa vyao. Nanyi waungwana, je mnatambua, nanyi ndugu zanguni, je, mnatambua hili, kwamba mnapolikataa jambo lile hasa ambalo Mungu analithibitisha mbele yenu, kwamba mnafanya jambo lile lile walilolifanya, kurudia matapiko ya mapokeo yenu?

¹³⁰ “Kama mbwa ayarudiavyo matapiko yake...” Kama yalimchafua moyo mara ya kwanza, yatamchafua moyo mara ya pili. Kama kanisa Katoliki lilipoundwa na kufanywa dhehebu la mwanzo lilileta ugonjwa kwa kanisa, ndivyo watafanya Walutheri, Wamethodisti, na wengine wote, Wabatisti, Wapresbeteria, na Wapentekoste. Mbwa anarudia matapiko yake na nguruwe anarudi kugaa-gaa matopeni. Mnaona? Tufafikia hayo katika dakika chache, Bwana akipenda.

¹³¹ Mng’aro, kutembea katika mng’aro (mnaona?), mazigazi, wazo bandia ya Nuru ya kweli. Alithibitisha kuwa Yeye alikuwa ile Nuru, kwa sababu Yeye akiwa katika ile—kule katika uchache (lo jamani!), mamilioni dhidi Yake. Hakukuwa sehemu moja katika sita ya watu, sehemu moja katika tisini ya watu duniani waliojua Yeye alikuwako. Sio nadhani moja—asilimia moja ya Wayahudi, au haifikii mmoja katika hamsini ya wao au arobaini ya wao, nitasema—pengine wachache kuliko hao—wa nchi Yake waliojua alikuwako. Na wale waliojua alikuwako, walimdhania kuwa kitu bandia, kwa sababu dhehebu liliwaambia alikuwa hivyo. Mnaona? Lakini hata hivyo Yeye alikuwa ile Nuru ya kweli ambayo ilikuwa imenenwa tangu Mwanzo kule mwanzoni, na akawauliza wayachunguze Maandiko waone kama hakuwa anaishi katika wakati huo, kama Yeye—zile kazi alizozifanya hazikutimiza yale hasa yaliyoahidiwa wakati huo. Amina!

¹³² Ni jambo nzito jinsi gani, ndugu. Tunaishi katika wakati wa ajabu sana. Alidhibitisha kuwa wa kweli.

¹³³ Alikuwa Nuru ile ile waliyodai walikuwa wanaiabudu. Walidai kuwa walikuwa wanaabudu Nuru hiyo. Na ndivyo ilivyo leo. Wanadai kwamba wanaabudu hiyo. Wapentekoste wanadai hivyo. Wanadai wanafanya hivyo, na ni vipofu mno hawaioni. Kwa nini? Walijifanya dhehebu na kuweka mng’aro katika nyuso zao. Mnaona? Mapokeo ni kitu watu waliketi pamoja na kusema, “Tutafanya hili, na hili, na, hili, lile.” Sasa, tutafikia sababu ya hilo kutendeka. Bwana akipenda.

¹³⁴ Angalia, kazi Zake zilikuwa Neno hai Lenyewe. Yale aliyofanya yalikuwa Neno hai Lenyewe, akionyesha Yeye alikuwa ile Nuru iliyoahidiwa tangu mwanzo wa ulimwengu. Alikuwa ile Nuru. Nuru Yake katika Neno lililoahidiwa la wakati huo ililifanya liishi sawasawa na yale ahadi ilisema litafanya, bali walikuwa wameligeuza sana mpaka hawangeliona. Mnaona? Bali alikuwa Nuru ya wakati huo.

¹³⁵ Alikuwa ile Nuru waliyodai kuwa wanaiabudu. Walidhani walikuwa wanamwabudu yule Mungu wa maumbile. Bali walikuwa wakiishi na kuabudu mng'aro, naye Yesu akasema, "Mwaniabudu bure, mkifundisha mafundisho yaliyo mapokeo ya wanadamu wala si Neno." Yeye ndiye Neno, naye alikuwa Neno likidhihirishwa. Walipaswa walijue. Natumaini hilo laweza kupenya kila linaposikizwa (unaona?), kuwa ni Neno likidhihirishwa.

¹³⁶ "Lo," kasema, "Lo, tunalo Neno!" Kwa nini, Neno, kila mtu anayetaka anaweza kubeba Biblia, bali wakati lile Neno linapothibitishwa, linadhihirishwa. . .

¹³⁷ Kwa nini, kasema, "Vema, tunaamini!" Ndiyo, bwana! Waliliamini Neno lote, vema, hata Shetani pia. Wale Mafarisayo, nani angewalaumu kwa kutokuamini? Bali hawakuliamini Neno la saa hiyo. Walikuwa wakiabudu katika mng'aro wa kitu kingine. Hivyo ndivyo wanavyofanya leo. Mnayashika mapokeo ya Luther au—au mapokea ya Wesley, na wengineo, mapokeo ya Kipentekoste, lakini je kuhusu saa hii? Mafarisayo walikuwa wakiyashika mapokeo yao, bali nyuma ya mapokeo yao lilikuweko Neno la Mungu likija kuangazia. Na lilipofanya hivyo, likapofusha macho yao. Hawangeliona, kwa sababu walikuwa wakitazama jambo lingine. Ndivyo ilivyo leo. Mungu na aruhusu hilo likolee, mpaka lieleweke kabisa na wale wanaopaswa kuliamini. Wakati umechelewa zaidi ya mnavyodhanja.

¹³⁸ Mwanangu, Billy Paulo, hunena katika usingizi, bali hapati ndoto mara nyingi. Aliota moja juzi usiku iliyomshtua. Kasema aliota kwamba alikuwa katika kanisa fulani, na—na wao—mimi nilikuwa sijaingia bado. Kasema nilipoingia, moto ulikuwa ukiruka kutoka kwa macho. Na nikasema, "Wakati umewadia; umekwisha!" Na kila mtu akaanza kupiga mayowe, "Siwezi, watoto wangu." Na hata. . .

¹³⁹ Mke wangu akasema, "Siwezi kumfanya Sarah aombe baraka mezani," na kadhalika. Nami nikasema. . .

Yeye akasema, "Lazima niende nimlete Loyce na—pamoja na mtoto."

¹⁴⁰ Nikasema, "Loyce hawezi kuja sasa. Mtoto ni mchanga sana hawezi kujua. Billy saa imefika; lazima tuende." Nikasema, "Ni usiku wa manane sasa, kabla hakujapambazuka Yesu atakuwa hapa. Kama sivyo basi mimi ni shahidi wa uongo wa Kristo."

Na mtu fulani akapaza sauti akasema, “Hakuna mtu ajuaye ile dakika wala ile saa.”

¹⁴¹ “Mimi sikusema dakika wala saa; nilisema wakati fulani kati ya sasa na mapambazuko.” Kisha nikasema, “Hebu—hebu twende, Billy.” Nami nikasema kitu. . . Nikasema, “Lakini tumefikia wakati huo, hebu twende.” Nasi tukapanda gari tukaondoka. Na tukaanza kupanda mlima. Na tulipofanya hivyo, ilikuwa—ilionekana kama kwamba nuru ilikuwa yaja, na anga zilikuwa na giza juu ya nchi. Alisema nilisimama kando ya barabara, nikainyosha mikono yangu hivi, moto ungali ukiruka kutoka macho yangu. Alisema nikasema, “Bwana, nimefanya haya kwa amri Yako. Nimefanya hivi tu kwa sababu Wewe uliniambia nifanye hivyo. Nimefanya haya kulingana na yale Wewe uliniambia.” Nami nikakielekeza kidole kwenye mlima mkubwa wa namna ya mawe magumu sana, na Nu—Nuru bila kazi ya mikono ikakata jiwe kutoka ule mlima lenye uzani wa tani mia kadhaa na hapa laja. Nikasema, “Geuzeni vichwa vyenu, msitazame. Yote itakwisha katika dakika chache.” Kasema, “Ndipo utulivu mkuu sana na mtakatifu ukaja kila mahali wakati lile jiwe lilipokuja likielekea mahali pale.”

¹⁴² Yawezekana wakati umepita zaidi ya tunavyodhanika. Kuna. . . Waona, hiyo ni kulingana na Maandiko hasa (mwaona?), lile Jiwe pasipo kazi ya mikono likikatwa kutoka mlimani. Na kwa hivyo hivi karibuni itakuwa hivyo mtakapolilia kitu fulani. Nikamwambia, “Tayari mmeshakuwa na wakati huo. Mungu kila mara amewaonya tena na tena.” Naam, nikasema, “Hata kama ni mwanangu mimi mwenyewe au yeyote yule, saa imewadia. Ninaweza kusema tu yale aliyoniambia niseme, na itakuwa hapa, na ikawa.” Na—na ndipo kwa ghafla hapa likaja jiwe lililokatwa kutoka mlimani pasipo kazi ya mikono. Danieli aliona hilo, mwajua, miaka mingi iliyopita. Na Billy hakujua lolote kuhusu hilo, bali ilikuwa—ilikuwa ndoto iliyotumwa kwake kutoka kwa Bwana.

¹⁴³ Sasa, mwaona, wanadai kuwa wanamwabudu Mungu yule yule ambaye walikuwa wanamfanyia mzaha. Na jambo lile limejirudia tena leo kwa sababu ile ile, kuishi katika mng’aro badala ya nuru. Nuru kuu zimeangaza. Sawa.

¹⁴⁴ Tazama giza gani tulilo ndani yake leo. Tazama yanayotendeka leo. Tazama mauaji, kulalana kwa sharti, ugomvi. Kwa nini, imetimia. . . Naamini ni Billy Graham aliyesema katika mkutano wake wa mwisho, “Katika muda wa miaka kumi tangu sasa kila raia wa California itamlazimu kubeba bunduki ya kujilinda nayo. Huwezi kuweka watunza sheria wa kutosha.” Watu wameingiwa na wazimu kabisa. Kupigana risasi, na mauaji, kulalana kwa sharti, kila kitu. Waona, kumechafuka (waona?) barabarani. Waona, ni—ni siku tunayoishi, siku ya Sodoma. Waona? Lakini kuna Nuru inayoangaza kama tu wangetazama, kama tu wangeona—

wangeangalia katika Neno na kuona yapaswayo kuwa katika saa hii, wangejua wanayojaribu kufanya.

¹⁴⁵ Sasa, wanadai kuwa wanaiaabudu ile Nuru. Ndivyo walivyodai kuwa walikuwa wakiabudu ile Nuru. Bali walikuwa wakiabudu katika mng'aro wa Nuru nyingine badala ya ile halisi. Unaona? Yeye alikuwa ile Nuru.

¹⁴⁶ Kanuni za imani na mapokeo na hali yao ya upofu viliwageuza kutoka kwenye Nuru ya kweli ya Neno lililoahidiwa. Lile Neno ambalo Mungu alilidhihirisha kwa Yesu aliye Nuru ya ulimwengu lilikuja na kufanya hilo Neno liishi sawa kabisa katika wakati Wake, sawasawa kabisa na siku hizo. Yeye atakatiwa mbali katikati ya majuma sabini (hiyo ni kweli), ambayo ni miaka tatu na nusu ya unabii Wake. Yule Masihi angekuja, yule mtawala, na atoe unabii. Na siku tatu na nusu za hii, ndipo angekatiliwa kutoka kwa walio hai na afanye upatanisho. Na hiyo ni sawa kabisa. Alihubiri miaka tatu na nusu, halafu. . .

¹⁴⁷ Na ile Zaburi ambayo Daudi alisema, “Mungu wangu, Mungu wangu, mbona umeniacha (Zaburi ya 22)? Mifupa yangu yote, wananikodolea macho. Wanatikisa vichwa vyao; wanapita karibu nami.” Miaka mia nane na hamsini mbeleni wakati Daudi aliuimba wimbo huo katika Roho, na ukafikiriwa kuwa unabii, na kutolewa. . . Walikuwa wakiziimba nyimbo hizo hekaluni wakati Sadaka ile ilikuwa inaning'inia msalabani mikono Yake ikiwa imechomwa, “Na wakachoma mikono Yangu na miguu Yangu.” Unaona? Unaona pale? Kwa nini? Walikuwa wakiishi katika mng'aro; hawakuiona ile Nuru.

¹⁴⁸ Ungewazia mtu mwenye busara akifanya hivyo? Si zaidi ya vile ninavyoweza kumfikiria mtu mwenye busara akikimbilia orofa ya chini na kuingia kwa nguvu na kufunga milango yote na kusema, “Sitaki kuona kuwa kuna nuru.” Ni wazimu. Na hali yake ya kiroho iliteleza mahali fulani, wakati mtu anapoonza kuwa Biblia imeahidi hili na alione likiwa hai mbele yake na kudhihirishwa naye aendelea kukaa katika hizo kanuni na mengineyo kule nje na kulikataa. Ni hatia ya kiroho. Hiyo ni sawa kabisa.

¹⁴⁹ Alikuwa hapa sasa. Alikuwa—Alikuwa Nuru ya ulimwengu, na ulimwengu ulijua. . . Alikuwa kwa walio Wake; wala walio Wake hawakumjua. Alijua ulimwenguni; ulimwengu uliumbwa naye, wala ulimwengu haukumjua. Waona? Bali wote waliomjua aliwapa uwezo wa kufanyika watoto wa Mungu, ndio wale waliomwamini.

¹⁵⁰ Kumbuka, hatuwezi kuishi kwa nuru ya jana. Nuru ya jana imeondoka. Haipo tena. I. . . Nuru ya jana ni kumbukumbu tu. Nuru ya jana ni kumbukumbu tu, au ni historia. Hatuwezi kuishi katika nuru ya jana. Si zaidi. . . Na vivyo hivyo. . . Ingawa ni

jua lile lile—jua lile lile—bali kila siku huleta nguvu zake zenye nguvu zaidi ili kuivisha nafaka kwa mavuno. Waona?

¹⁵¹ Jua likija leo, linakuwa na nguvu zaidi kidogo. Kila siku sasa, litakuwa na nguvu zaidi kidogo, nguvu zaidi kidogo, mpaka hatimaye ile ngano inayolala pale, ita—itatwaa uhai. Baada ya kitambo kidogo uhai utatokea. Halafu iwe na nguvu zaidi kidogo, nguvu zaidi kidogo. Machi, Aprili, Mei, Juni, Julai, imefika katika mavuno wakati huo. Mwaona? Jua lile lile linaloangaza leo katika—katika Januari—au Desemba, lilipo pale juu likiisafisha hiyo theluji na kuiyeyusha chini juu ya hiyo punje, kuiletea maji, ni jua lile lile, lakini ile ngano haingeishi katika nuru ile ile ya jua katika Juni. Waona? Haiwezi. Mnaona, jua huja na nguvu zaidi kidogo kila siku. Na hiyo punje yapaswa kuwa imekomaa zaidi kidogo kupokea nuru ya jua.

¹⁵² Hiyo ndiyo shida leo. Punje iliyopandwa katika baba wa kwanza kule nyuma katika—katika Luther na Wesley na wengineo, ilikoma kukua iwe kubwa, haiwezi kupokea jua. Jua linaiuwa. Ilikataa kukua. Mnaona? Ilijikata—ilijitoa kutoka ubua na kuja hapa na kujitengenezea vitu vidogo, ikawa ganda wakati huo, hamna uhai ndani yake. Punje inapaswa kuendelea kukomaa na kuzidi kuwa na nguvu jua linavyoendelea kuwa na nguvu kila siku.

¹⁵³ Sasa, na tuangalie kwa dakika moja. Tutaangalia nyakati za kanisa. Kuna nyakati saba za kanisa. Katika nyakati hizo za kanisa, kila mmoja, tazama jinsi Yeye alivyowaeleza yatakatotendeka, jinsi ile punje ingekomaa hata kufikia hii saa ya mwisho hapa; hii saa ya mwisho tunayoishi. Basi makanisa lazima yafanye jambo lile lile (mwaona?) makanisa.

¹⁵⁴ Sasa angalia, Luther alipanda punje moja, na Luther alikuwa punje moja. Kisha akaipanda. Sawa. Wesley pia, vivyo hivyo Wapentekoste pia. Vivyo hivyo Batisti pia, Nazarine. Lakini, waona sasa, Luther hangerudi nyuma na aishi katika nuru ya dhehebu la kwanza, Katoliki. La, bwana! Yeye alikuwa nuru nyingine. Huyu alikuwa Mungu akiivisha kitu fulani.

¹⁵⁵ Sasa, wachache kabisa walitoka katika ule—ule ufufuo wa Luther. Halafu ukaja ufufuo wa Wesley. Na ndipo katika huo, kwani, hawangerudi nyuma na kufanya Walutheri. Waona? Kisha wakaja Wapentekoste, halafu Wapentekoste wakajifanya dhehebu na kufanya jambo lile lile, wakachukua kapi. Angalia, lakini ile punje yaendelea tu mbele.

¹⁵⁶ Sasa, tuko katika wakati mwingine. Mbona wasilipokee? Mbona wasione kwamba punje imekomaa? Hapa kuna Neno lililoahidiwa siku hii. Mbona hawalioni? Kwa sababu wanaishi katika mng'aro wa Luther, mng'aro wa Wesley, mng'aro wa Wabatisti, mng'aro wa Kipentekoste. Wanaishi katika mng'aro wa nuru nyingine. Hiyo ndiyo sababu hawawezi kupokea Nuru ya Neno kamili likidhihirishwa kama Mungu alivyoahidi juu

ya zile Muhuri Saba, ambapo siri yote ilifunuliwa, ingerudi na kueleza kwa nini siri hizi zote zilifanywa hivyo. . . Na hata hivyo hiyo inapoingia, wanatembea mbali zaidi kutoka kwayo kuliko hapo mbeleni. Hawana udhuru.

¹⁵⁷ Mungu amefanya hilo kupitia roho, kupitia funuo. Yeye ame—amelithibitisha kikamilifu kwa sayansi na kadhalika kwamba hiyo ni Kweli—kwamba hiyo ni Kweli. Na bado wanataka kuishi katika mng'aro wa Kipentekoste: “Mimi ni wa Assemblies”; “Mimi ni wa Umoja”; “Mimi ni wa Kanisa la Mungu”; “Mimi ni hili.” Mnaona? Kuishi katika mng'aro wa nyakati za miaka arobaini, hamsini iliyopita. Kuishi katika mng'aro wa Kiluteri, kuishi katika mng'aro wa Kiwesley, Kibatisti, Kipresbeteria, au mng'aro wa Kinazarine wa wakati mwingine wa kanisa uliopita na ukaunda dhehebu na kufanya jambo lile lile, na kukataa na kukana ile Nuru ambapo kwa kweli inaangaza. Na mnaishi katika mazigazi.

¹⁵⁸ Nasema haya kwa kicho (mnaona?), lakini ninyi—sio kuwaudhi, bali kuwaamsheni. Mnaishi katika mazigazi ambapo Yesu alisema, “Kwani, mu vipofu na mnaongoza vipofu.” Na wao. . . ? . . . Yeye alijaribu kuwaambia waiachilie. “Waacheni wao wenyewe. Kipofu akimwongoza kipofu, wote wataangukia shimoni.” Na hiyo ndiyo saa ambayo nimefikia. Ikiwa watayumbayumba, siwezi kuwazuia. Nimefanya yote niwezayo. Nimefanya sawasawa. . . Nimefanya hili kwa amri yako, Bwana. Wewe u shahidi. Tangu 1933 pale chini mtoni wakati ile Nuru mnayoiona ilianga; Imekuwa papa hapa katika maskani na kuwashuhudieni nyote miaka hii yote. Na kila kitu iliyosema kilitimia. Na daima wanaendelea. Acheni vipofu wawaongoze vipofu. Mimi nitaingoja tu saa hiyo. Atawasili mojawapo wa siku hizi.

¹⁵⁹ Angalia, kuishi katika mng'aro wa Luther, kuishi katika mng'aro wa Wesley, kuishi katika ile ming'aro kule nyuma, hiyo ndiyo sababu hawawezi kuona Nuru ya kweli. Kama wangekoma kwa dakika chache na kuichukua Biblia na kuisoma, wangeona kwamba ile—hii ni Nuru iliyoahidiwa kwa saa hii.

¹⁶⁰ Sasa, tutayachukua baadhi ya mambo haya hivi punde. Yeye aliahidi kulingana na Malaki 4 mambo haya yatatendeka. Yeye aliahidi kote Maandikoni kuwa yangetendeka. Mnaona?

¹⁶¹ Angalia Israeli pia, mfano wetu, katika ile safari (tazama!) wakila mana iliyokuwa kwao uzima-nuru, iliyowapa nguvu, uzima. Hiyo ni kweli? Israeli hawangekula mana iliyoanguka jana. Ilikuwa imeharibika; ilikuwa imeoza. Haikuwa nzuri kwao; ingewaua. Mana iliyowadumisha hai jana ingewaua leo. Biblia ilisema ilikuwa na viini vya magonjwa, imeharibika. Na ile mana. . . Iliwabidi kupata mana mpya kila siku. Amina! Na ni nini? Watu wanaoishi kwa mana ya Luther, Wesley, na wengineo

kule nyuma, mnakula kitu kilichoharibika kinachowaua kiroho. Mnaona? Kinawaua, mmekufa katika mapokeo yenu.

¹⁶² Ya jana, mana ya Luther haingewafaa Wamethodisti. Mana ya Kimethodisti haingefaa kwa Wapentekoste. Mana ya Kipentekoste haitafaa kwa siku hii. Mwaona ninayomaanisha? Kila siku ilikuja siku baada ya siku, mpya, na ndivyo ipasavyo kuwa katika nyakati za kanisa. Mana ya Luther ilikuwa ujumbe wa kuhesabiwa haki. Ujumbe wa Wesley ulikuwa dhihirisho la utakaso. Upentekoste ulikuwa kurejeshwa kwa karama. Bali huu ni kulijulisha Jiwe la Kuwekwa Juu Kabisa, siku ya mwisho, Mti wa Bibi-arusi. Ni kinyume cha yote hayo. Na hata hivyo ni Nuru ile ile kwa waliokomaa, kama vile lile jua linaloangaza leo litaivisha nafaka kwa ajili ya mavuno mwezi wa Julai. Mwaona ninayomaanisha? Bali Nuru ya leo haitafaa lolote kule nyuma Julai. Ina nguvu zaidi; ngano imeendelea zaidi. Iko tayari kulipokea. Amina! Hakika iko hivyo. Haingelipokea sasa. Wakati huo italipokea. Majira hayakufaa wakati ule; sasa yanafaa.

¹⁶³ Huwezi kuyapinga maumbile ya Mungu. Yeye ana sheria. Na kuipinga hiyo sheria huangamiza mmea wako. Lazima uambatane na sheria zilizonenwa za Mungu, na sheria Zake ni Neno Lake. Sheria yoyote ni neno lililonenwa. Na neno ni wazo lililodhihirishwa. Unaona?

¹⁶⁴ Sasa, tu—tunajua hayo; hiyo ni kweli. Ono ni nini? Neno la Mungu, au jambo lililotabiriwa au kubashiriwa kwa tukio fulani. Na ono ambalo manabii walikuwa nalo, Yesu alilokuwa nalo, alilokuwa nalo Paulo, na wengine wote linalonena kuhusu siku hii lilikuwa utabiri wa yale ambayo yangetendeka. Na hapa twaona utabiri ukidhihirishwa, na watu hata hawautambui. Mwaona ninayomaanisha?

¹⁶⁵ Sasa, mana ya jana...Angalia hapa! Je, umeshawahi kuona jua—j-u-a—lmesafiri kutoka mashariki hadi magharibi kama lilivyoendelea kila wakati. Mlitambua hayo? Na tazama, nyakati za kanisa zilifanya vivyo hivyo. Nini...Jua—m-w—j-u-a lilianza mashariki. Na ustaarabu umeandamana na jua, nuru iliyonenwa ya Mungu ili wao waishi kwayo. Wameendelea, wamelifuata jua, kuona lilikokuwa linaenda.

¹⁶⁶ Maisha yenyewe ulipozaliwa ni kama jua. Unaendelea moja kwa moja hadi kutua kwa jua, tangu kuzaliwa kwako hadi kutua kwa jua.

¹⁶⁷ Mwanadamu amesafiri magharibi daima. Ustaarabu wa kale kabisa tulio nao ni China katika nchi za mashariki, Yerusalemu...Na tazama, unaendelea kusafiri magharibi kama uendavyo. Na unavyoendelea na kuendelea magharibi, ndivyo wakati wa kanisa umesafiri vivyo hivyo kwa M-w-a-n-a wa Mungu.

¹⁶⁸ Angalia! Paulo... Kanisa la kwanza lilianza mashariki; likatoka pale, likaruka ba—ba—bahari mpaka Ujerumani. Na limefanya mivuto mitatu. Tazama. Kutoka Asia kule chini katika—katika Palestina liliruka bahari mpaka Ujerumani. Huyu alikuwa Luther. Na liliruka kutoka Luther kuvuka Mlangobahari wa Uingereza likaingia Uingereza kwa Wesley. Na kutoka Wesley limeruka hadi Pwani ya Magharibi ya Marekani. Na hii, ukienda mbele zaidi linarudi mashariki tena. Huu ni wakati wa jioni!

¹⁶⁹ Tazama jinsi nyakati za kanisa zimeshuka... Luther... Paulo kwanza kule katika nyakati za mwanzoni, halafu likashuka chini kumfikia Irenia na kadhaliika, likaendelea hata Ufaransa. Kutoka pale likaingia Ujerumani, likaingia Uingereza, daima likienda magharibi. Na sasa hatuwezi kuenda mbele zaidi. Huu ndio wakati wa mwisho! Na Biblia inasema nini kuhusu wakati huu wa mwisho? Mnaona, kigeografia, jinsi mambo yanavyofuatana, na karibu kila namna upendavyo kulichukua, Kimaandiko kwanza. Bila shaka Maandiko kwanza, ushahidi, kihistoria, namna yoyote upendavyo kulichukua, tumefika mwisho, wakati wa mwisho wa kanisa.

¹⁷⁰ Na tazama, kama lilivyoendelea mbele ndivyo lilivyo zidi kukua katika nguvu. Vivyo hivyo pia lile kanisa dogo la wachache limekua kutoka Kuhesabiwa Haki, Utakaso, Ubatiso wa Roho Mtakatifu, na sasa kuja kwa lile Jiwe la Kufunika, likijipatia umbo. Hamna madhehebu zaidi baada ya hili. Hakutakuweko na mengine. Unaona? Haiwezekani. Waona, tumefika magharibi.

¹⁷¹ Kuwaonyesheni tu, kupitia mifano yote na kila kitu kingine. Na tazama hiyo miruko mitatu, mivuto tatu. Tutaingilia hayo usiku huu (mwaona, mwaona?), jinsi tulivyo katika wakati wa mwisho. Ni tu... .

¹⁷² J-u-a limesafiri kama M-w-a-n-a; M-w-a-n-a kama j-u-a. Kanisa limekuja vivyo hivyo kutoka zile Nyakati Saba za Kanisa na kadhaliika. Ustaarabu umeendelea kufikia magharibi, na kanisa limesonga mbele hata likafikia magharibi. Na sasa, tukienda mbele zaidi ya pale tulipo sasa, tutarudi mashariki tena. Ukiondoka Pwani ya Magharibi utarudi moja kwa moja hata China, Japan, kule nyuma tena. Kavuka maili elfu saba kule unarudi mashariki tena. Basi mashariki na magharibi zimekutana. Hiyo tu. Tuko mwisho. Hakuna kilichosalia.

¹⁷³ Na jambo hilo hilo limetendeka leo, lililotendeka kule nyuma. Jambo lile lile limekutana magharibi lililokutana mashariki: watu wakiishi katika mng'aro wa nuru nyingine ambayo kwa kweli ilikuwa ikijaribu kuonyesha ile Nuru iliyokuwa ije na kuikataa, kwa vile walipata mng'aro badala ya Nuru. Lo! "Na kulikuwa na Nuru kuu katika nchi ya Mataifa, Zabuloni, Naftali ya—na Galilaya, nchi ya Mataifa."

¹⁷⁴ Huu ni Wakati wa Saba wa Kanisa. Kumbuka, na kila wakati ambapo lile jua lilianza kuangaza mashariki ni jua lile lile linaloangaza magharibi. Na Roho yule yule ambaye amekuwako katika nyakati zote namna hiyo ni jua lile lile leo, ila tu ni nini? Ni kama tu kukomaa katika majira. Ju—jua lililopo sasa ndilo jua lile lile liivishalo punje majira haya ya kupukutika, majira ya masika. Mnaona? Lakini ni nini? Ni jua hili pamoja na kile litakuwa. Na leo katika wakati huu wa mwisho ni kile walichokuwa kuongeza hiki. Na hata hivyo wangependa waishi kule nyuma kama mbilikimo, wateremke hadi mahali pa kale—pa kale penye kutu—orofa ya chini ya kidhehebu na kanuni za imani na kufunga pazia zao na kusema, “Sitaki kuliona, lote ni upuzi.” Huku Biblia ile ile wanayodai kuia mini inapodhihirishwa na Roho Mtakatifu yule yule, ikileta Nuru katika siku za mwisho.

¹⁷⁵ Je, uliona... Na tazama kwa makini sana katika Malaki jinsi alivyopanga kuwa, “Imani ya akina baba kwa watoto wao na watoto kwa akina baba”? Waona, Roho yule yule mahali alipoinuka kule nyuma, anapoinuka hapa tena, jambo lile lile...? Waona, ni vinginevyo kabisa, ni kurudi tena. Kwa nini? Mashariki na magharibi zimekutana. Unaona, sawasawa kabisa machoni petu, na bado hawalioni. Kwa nini? Si ajabu Yesu alisema, “Waacheni peke yao, wao... Kipofu akiongoza kipofu, wote wataangukia shimoni.”

¹⁷⁶ Nuru ya nyakati zingine ilikuwa tu ikirudisha Nuru hii. Waona? Jua leo hurudisha tu nuru—ni kurudishwa kwa nuru ya jua litakalokuweco Julai hii au Agosti kama Mungu... kwa ajili ya mavuno. Na jua la Luther, Martin Luther, na Wesley, na Sanky, Pinney, Knox, Calvin, Moody, wale wengine wote hao watu wakuu kule nyuma waliokuwa na zile nuru; na John Smith wa kanisa la Kibatisti, na Alexander Campbell wa kanisa la Campbell au wanaoitwa Wanafunzi wa Kristo, kanisa la Kikristo, na majina mengine waitwayo; watu hao wote kule nyuma katika nyakati zao walikuwa wakirudisha tu nuru ya yale ambayo yangekuweco hapa wakati wa mwisho.

¹⁷⁷ Na basi hapa, watoto, mara baada ya wale waanzilishi, wanafanya nini? Hawakukaa katika ubua. Waliondoka na kujifanyia kitu kama ganda dogo hapa nje ambapo unatoka kwa chanzo cha uzima na huna uzima. Toa kapi kwa hicho kitu na ukipande nje huko ardhini, kitakaa hapo na kuoza. Vivyo hivyo mnajaribu kula mana iliyoza kutoka huko nyuma katika siku hizo. Mavuno yameiva. Yesu ana meza imeandaliwa ambapo watakatifu wa Mungu wanalishwa chakula kilichoiva cha siku hii, kwa Nuru ya Injili inayoidhihirisha...?...kwamba Yeye Yupo hapa leo. Watakatifu wanakula mkate.

¹⁷⁸ Fikiria tu. Ganda zee la jana (mnaona?), usilipande kule nyuma; limeoza. Haliwezi—haliwezi kukaa nalo. La, bwana! Halitafaa kitu; halitakua. Limeondoka kwa ule uzima. Na Neno

ndilo Uzima. Hiyo ni sawa. Ganda linaanguka, kile kidevu kizee kinaanguka, mambo kama hayo; linajifanya dhehebu na kuanguka. Linakataa kuendelea mbele na Uzima. Bali Nuru inalithibitisha. Lo, jamani! Ndiyo, Bwana! Ya jana... Lo, jamani!

¹⁷⁹ Jinsi itupasavyo kuona hivyo, kuona kwamba vitu vilivyooza vya jana, tusivile leo. Mnaona? Vina mabuu. Mnawajua hawa ninaowaita wafurukuta mikia wadogo? Sijui, sijui sana kuhusu maisha ya hawa mabuu, bali najua daima tuliwaita wafurukuta mikia. Huingia katika kitu chochote kinapooza kidogo. Mnaona? Sikitaki wakati huo. Kama watosheka nacho, endelea. Lakini sio mimi.

¹⁸⁰ Lakini kumbuka... Unasema, “Basi mbona ilikuwa nzuri jana?” Kama ungejua tu kuwa lile ganda ndogo lililokuwa katika ngano mwanzoni, kama likikaa katika ile punje, linaifanya punje kukua zaidi. Hilo ndilo jambo lile linalofanya ngano ichanue na ndilo lililokuwako jana. Bali likijitenga na ngano na lisikomae, basi linaondoka. Mnaona? Bali likipitia katika njia ya utaratibu unaotoa uzima linapokufa, linageuka kuwa kitu kingine na kufanya punje. Kama si hivyo, inatoka wapi? Amina! Mwaelewa?

¹⁸¹ Kama vile Malkia wa Uingereza wakati mmoja, alienda kwa kampuni kubwa ya karatasi. Basi alisema angependa kukizuru kiwanda cha karatasi. Basi wakamuonyesha kinu cha karatasi (miaka mingi kabla hawajaanza kuiseta na kadhalika, basi wali—wakitengeneza karatasi kwayo), basi wao... Baada ya kitambo kidogo akafika katika chumba ambacho hakikuwa kitu bali fungu kuu zee la matambaa machafu, akasema, “Haya yalitoka wapi? Hii ni nini?” “Lo,” akasema.

Yu—yu—yule rais wa kiwanda akasema, “Hii ni—ndiyo itatengenezwa karatasi, haya matambaa machafu.”

Akasema, “Hayo, eti yatengeneze karatasi?”

¹⁸² “Ndiyo!” Basi ilikuwa shida kwake kuamini. Basi baada ya kuondoka, yule mtu akachukua lile fungu la matambaa machafu, na kuyapitisha katika hatua fulani, na kuyatoa yakiwa karatasi safi, nzuri, mwajua, yalikuwa—yakapitia hatua fulani na kufanywa halisi, na kuweka picha yake ndani yake, na kumpelekea malkia ikionyesha picha yake katika yale aliyoita matambaa machafu.

¹⁸³ Sasa, hivyo ndivyo ilivyo, vitu vilivyokufa vya jana, ujumbe wa Luther, ujumbe wa Wesley, ujumbe wa Pentekoste, kama tu ungepitia katika hatua ya Roho Mtakatifu wa Mungu na Neno lililothibitishwa, utaleta sura ya Mfalme Yesu Kristo. Amina! Bali ukiuacha ulale, ni matambaa machafu. Mnaona? Lazima ufinyangwe uwe kitu kingine.

¹⁸⁴ Luther lazima afinyangwe awe Wesley, na Wesley lazima afinyangwe awe Pentekoste, na Pentekoste lazima ifinyangwe

iwe Kristo. Zinapitia katika hatua fulani. Kadhalika na Injili imepitia katika hatua. Ni kupitisha katika hatua. Wakati wa Luther wa kuhesabiwa haki, tunaamini hiyo. Wa Wesley wa utakaso, tunaamini huo. Wapentekoste na kurudishwa kwa karama za Roho Mtakatifu, tunaamini hivyo. Hakika, bali yafinyange yote pamoja, utapata nini? Yesu (sawa!) yeye yule jana, leo, na hata milele. Utapata Yesu.

¹⁸⁵ Wakati mtu katika kiwanda cha kufua chuma anatengeneza kengele, yeye ana mlio fulani ambao ameweka ndani yake. Anapoweka kalibu yake na kumwaga chuma ndani yake, anatia shaba nyeupe kiasi fulani ndani yake, chuma cha pua kiasi fulani, shaba kiasi fulani, kwa nini? Anajua sawasawa kiasi gani cha kuweka katika—kufanya—kuipa mlio sawa. Na hivyo ndivyo Yesu amefanya kwa Bibi-arusi Wake. Ilimbidi aweke kiasi fulani cha Luther, kiasi fulani cha Umethodisti, kiasi fulani cha Presbiteria, kiasi fulani cha Pentekoste ndani yake, lakini hatimaye anapata nini? Sura Yake mwenyewe. Kwa nini ni hivyo? Ni sawasawa na ujumbe wa piramidi. Waona, lajipanga kuendelea juu mpaka kufikia uchache kwa ajili ya Jiwe la kufunika. Huduma ya Yesu Kristo duniani lazima ifanane na ile aliyokuwa nayo, la sivyoye, Yeye hatakuja kwake. Ni kama tu kichwa kwa miguu. Kichwa, miguu si kichwa, bali kichwa huibeba miguu, au huifanya miguu, kinaambia miguu mahali pa kuenda. Mnaelewa? Nzuri kabisa, ni Nuru ya wakati huu.

¹⁸⁶ Wesley alikuwa Nuru kuu, kama yeye alivyosema kwa Yohana Mbatizaji. Alikuwa Nuru kuu kwa saa yake, hakika alikuwa.

¹⁸⁷ La—ndiyo, bwana! Matambaa safi—au matambaa machafu ya jana, ukikaa hivyo lazima yata—yatakuwa tu matambaa machafu daima. Yalitumikia kusudi lao kama mavazi, lakini sasa yamekuwa karatasi. Kuhesabiwa haki kulitumikia wakati wake katika kuhesabiwa haki chini ya Luther, halafu ilibidi iwe utakaso kupitia Wesley. Na utakaso ulitumikia wakati wake mpaka ukaja ubatizo wa Roho Mtakatifu. Na ubatizo wa Roho Mtakatifu umetumikia wakati wake mpaka Roho Mtakatifu—ambapo kuna Mungu mmoja tu—anaungana na Kanisa, au Kanisa, au Kanisa linaungana na Kristo, hilo linamfanya Yesu Kristo aonekane duniani, yale aliyoahidi hapa katika Biblia. Pengine hutaamini hilo. Siwezi kukufanya uamini. Mimi ninahusika tu na Neno. Waona? Hiyo ni sawa.

¹⁸⁸ Basi unaona hiyo? Unaona hiyo? Kama unaona, itakuwa kama—mtu mmoja wakati fulani alienda—alienda Wales wakati wa ufufuo wa Welch. Kundi la watu walienda kule kutoka Marekani. Basi wakashuka wakaenda, wakasema walitaka kujua ni katika jengo gani walikuwa na huu ufufuo wa Welch. Wengi wenu mnakumbuka ule ufufuo wa Welch, ufufuo mkuu ulizuka miongoni mwa—mwa watu wa Welch huko Wales. Basi hawa watu, hawa wahudumu wakuu mno

na kadhalika wakatoka Marekani, wale—madaktari wa dini. Walitaka waende waone ni jambo gani kubwa walilofanya, mwajua. Basi walikuwa wakiteremka barabarani na kusema—wakakutana na askari mdogo mzee aliyesimama pembeni akizungusha fimbo yake, mwajua, a—akiimba kwa kupiga mbinja, hivyo; wakasema; “Lo, yeye anaimba tu kwa mbinja. Pengine tumwendee, tumwone, tuone atafanya nini—tumuulize swali.” Basi wakamwendea na kusema, “Bwana, ufufuo wa Welch uko wapi?”

¹⁸⁹ Akatoa kofia yake; akasema, “Mabwana, ufufuo wa Welch uko hapa ndani!” katika moyo wake. Lo, ndiyo hiyo; yeye alikuwa ufufuo wa Welch. Ee, Mungu, laiti tunge—tungeelewa tu kuwa sisi ni sura ya Yesu Kristo, Neno Lake likidhihirishwa. Ninyi ni dhahirisho la Neno Lake. Unaona?

“Ufufuo wa Welch unafanyika wapi? Umo katika jengo gani?”

Akasema, “Bwana, uko moyoni mwangu.” Alikuwa ufufuo wa Welch. Hiyo ni kweli.

¹⁹⁰ Na leo kanisa lapaswa kuwa Yesu Kristo katika matendo duniani. “Kwa vile ninaishi, nanyi mtaishi pia; na uzima Wangu utakuwa ndani yenu. Kazi nizifanyazo Mimi, ninyi nanyi mtazifanya.” Mnaona? Kanisa halina budi kufika pale ili... Na Yeye aliahidi litafanya hivyo, na litafika. Lazima lije hivyo. Basi unaona, hiyo ndiyo inatendeka. Sisi—sisi lazima tuwe hivyo.

¹⁹¹ Yeye ni Nuru. Vivyo hivyo Nuhu alikuwa Nuru katika siku yake. Alikuwa Nuru. Nuhu alikuwa ile Nuru. Alikuwa Nuru kwa nini? Kulifanya Neno la Mungu. “Nitamwangamiza mwanadamu niliye muumba katika dunia. Jenga safina, na wote wapendao kuingia ndani yake wataokoka.”

Nuhu akaenda pale nje akasema, “Kuna njia moja, na hiyo ni safina.”

¹⁹² Wakasema, “Yule mzee, wazimu na mwenye kichaa.” Yeye alikuwa Neno lililodhihirishwa! Nuhu alikuwa Nuru ya saa ile, hakika alikuwa hivyo. Katika siku yake, alivangazia wakati wake Nuru.

¹⁹³ Musa alikuwa Nuru ya saa yake. “Hakika nitakuzuru,” Mungu alimwambia Ibrahimu. “Nitashuka, na nitawatoa kutoka—watu kwa mkono wenye nguvu; nami nitaonyesha nguvu Zangu katika Misri.” Na wakati Musa kule juu alikutana na kile kijiti kilichowaka moto kule juu na kuona kuwa MIMI NIKO alikuwa katika kile kijiti, Musa aliteremka kule chini, naye alikuwa ndiye Nuru. Amina! Si ajabu angechukua mavumbi ayapulize na kusema, “Viroboto na viwe juu ya nchi.” Alikuwa na Neno la Mungu. Nini ilitendeka? Mavumbi yalianza kupeperushwa, na viroboto vikaanza kuweko. Haleluya! Kwa nini? Yeye alikuwa dhahirisho la Nuru ya Neno la Mungu,

“Nitaipiga Misri.” Yeye alikuwa nabii. Aliyosema yalitimia. Yeye alikuwa Nuru ya siku hiyo. Alikuwa Nuru ya Mungu.

¹⁹⁴ Farao angekuwa na vyote ambavyo angependa kuwa navyo, na wote wengine wote, makuhani wote walikuwa na walivyotaka, bali Musa alikuwa Nuru. Kwa nini? Alikuwa akionyesha Neno la Mungu likidhihirishwa. Mungu aliahidi, “Nitawatoa kwa mkono wenye nguvu, na nitajipatia utukufu.” Hayo ndiyo alikuwa anafanya. Hiyo ndiyo sababu Musa alidhibitisha kuwa anaweza kuumba, si kwa sababu alitaka kuumba, kwa sababu Mungu alimwambia afanye hivyo...?... Nenda kwa kusanyiko, kasema “Kesho...Bwana Mungu amesema nami sasa hivi. ‘Chukua mavumbi mkononi uyatupe juu angani hivi na kuviita vije. Hakuna hata kimoja hapa, bali vitakuwepo.’” Amina! Lo, natumaini hamjalala. Lo, dhihirisho.

¹⁹⁵ Alisema, “Nimetumwa. Mungu aliwaambia baba zetu hakika angetuzuru hapa chini na kututoa. Nimekuja kuwathibitishia kuwa ile saa imefika. Tupeni mliyo nayo. Hebu tuendeni.”

¹⁹⁶ Baadhi yao walisema, “Vema, naamini...” Dathani alisema, “Sidhani kuna haraka yoyote. Haitupasi tusingimshwe na hili, na ilionekana kwamba lilishindwa mara nne au tano.” Lakini hata hivyo, liliendelea.

¹⁹⁷ Walifikiri...Walitoka na kusema, “Tumpige huyu Musa mawe na kumwondoa kwetu; hatumtaki katika kundi le—letu hapa.” Musa aliendelea tu hata hivyo, kwa sababu alikuwa ile Nuru. Alikuwa Nuru ya saa ile. Kile alichokuwa nacho, kilikuwa nini? Mungu akidhihirisha Neno Lake lililoahidiwa kupitia kwa Musa, na Musa alikuwa Nuru.

¹⁹⁸ Elijah alikuwa Nuru. “Nenda kule nje ukakae kilimani; nimewaamuru kunguru wakulishe.” Amina!

¹⁹⁹ Ndiyo, Bwana! Alishuka akarudi na, “BWANA ASEMA HIVI, hata umande hautaanguka kutoka mbinguni hata nitakapouagiza.” Amina! “Pengine jua litaangaza, huenda mkaagiza mawingu na mfanye lolote mpendalo, bali hata umande hautakuja mpaka nitakapouagiza.” Alikuwa nini? Ile Nuru. Haleluya! Alikuwa Nuru, ile Nuru; alikuwa Neno la Mungu lililodhihirishwa.

²⁰⁰ Walifikiri alikuwa na wazimu akiketi pale juu. Alikuwa na wachukuzi waliomlisha, na wao wakiwa na njaa nusura kufa. Walitaka kuishi katika mapokeo, na waendeleo. Sio Musa—au sio Eliya, yeye alikuwa anaishi katika Nuru. Akiketi pale kandokando mwa kijito cha Kerithi na akiwa na wakati mzuri, na alikuwa na vyakula na mtu wa kumtumikia na kila kitu. Walifikiri alikuwa wazimu, bali alikuwa—yeye alikuwa Nuru.

²⁰¹ Wakasema, “Aisee, nini kilimpata yule ajifanyaye mtakatifu anayevingirika hapa? Mwajua nini, fulani alikuwa akiwinda juu; na akasema walimwona amesimama pale juu karibu na—

kule juu ya ule mlima kule. Nina hakika yule mzee karibu amekauka sasa.” La, hashu! Alikuwa Nuru. Alikuwa Nuru. Alikuwa Nuru ya Mungu ya siku yake.

²⁰² Yohana, alipokuja duniani na, akatoka na kuenda nyikani apate elimu yake kutoka kwa Mungu, sio kutoka seminari, ilimbidi amjulisha Masihi...Basi alipojitokeza Yesu alisema alikuwa Taa angavu inayong’ara. Haleluya! Kwa nini? Alikuwa Neno lililodhihirishwa. Isaya alisema hivyo...?...Hiyo ni kweli. Angetuma sauti nyikani iliayo, ikisema, “Itengenezeni njia ya Bwana, mkalinyoshe lango Lake—inyosheni njia.” Analia, mmoja... Sauti ya mtu aliaye nyikani, hapa yuaja. Alikuwa ni nini? Sauti ya mmoja aliaye nyikani. Alikuna nini? Dhihirisho la Neno, Nuru. Mungu yule yule aliyenena katika Mwanzo aliyesema hili, na hapa kukaja uzima. Kama alivyosema, “Iwe nuru kwa jua,” jua likawa, vivyo hivyo alisema kutakuwa na sauti ya mtu aliaye nyikani. Hapa akajitokeza. Ilikuwa Nuru ya saa ile.

²⁰³ Alisema pia katika siku za mwisho (amina!), Nuru ya wakati, ikilia katika nyika ya Babeli, “Tokeni kwake, enyi watu Wangu, msishiriki dhambi zake. Msiguse kitu chake kilicho kichafu; jitengeni nacho. Itorokeni ghadhabu ijayo.”

²⁰⁴ Yohana alisema jambo lile lile: “Shoka limekwisha kuwekwa penye shina la mti.” Hata hakuwa na elimu, hata hakunena kama mhubiri. Alizungumza kuhusu nyoka, na vijiti, na miti, na mashoka, na mengineyo, yale aliyoyazoea nyikani. Hakukuzwa katika mambo haya makuu, makubwa, mazuri waliyo nayo leo, na yale waliyokuwa nayo siku hiyo. Alitoka na lugha yake mwenyewe. Hakusimama na kusema, “A-a-mina!” na kuinama huku kote kipuzi. Alikuwa moja kwa moja kutoka—kutoka nyikani akivaa ngozi na mkali, kasema, “Usianze kufikiri kwamba, ‘Mimi ni wa *hili*, mimi ni wa *lile*.’ Katika mawe haya Mungu aweza kumwinulia Ibrahimu watoto.”

²⁰⁵ Usifikiri eti kwa vile u Mmethodisti, Mbatisti, Mpresbeteria kwamba unashikilia chochote kwa Mungu. Mungu anaweza kuwachukua walevi au makahaba kutoka mitaani na kuwafanya watakatifu. Kuna mtu atakayelisikia, kuna mtu atakayeliadini.

²⁰⁶ Pia alisema, “Shoka limekwisha kuwekwa penye shina la mti, na kila mti usioadini hukatwa na kutupwa motoni.” Basi huo ndio ulikuwa ujumbe wake. Alikuwa Nuru ya siku ile.

²⁰⁷ Yesu alisema, “Yeye alikuwa Nuru angavu inayong’ara na ninyi kwa kitambo kidogo mlitamani kutembea ndani yake.”

²⁰⁸ Na Yahona alisema nini, yule nabii? “Yeye amesimama miongoni mwenu sasa hivi. Mimi sistahili kufungua viatu vyake. Na mara tu atakapojitokeza, mimi nitaondoka.” Lo jamani! Kwa maana Yeye alikuwa Nuru. Hakuna nuru mbili au tatu, hakuna madhehebu manne au matano tofauti, kulikuwa na Nuru moja. Hakuna Mmethodisti, Mbatisti, Mluteri, Mpresbeteria, Kristo

ndiye Nuru, nayo Nuru ndiyo Neno. Na Neno likidhihirishwa ndilo Nuru ya wakati huo. “Iwe nuru, ikawa Nuru.” Ndio, bwana! Iwe nuru, na kuna nuru.

²⁰⁹ Alisema kutakuwa na Nuru katika siku hii, na kuna Nuru. Yeye yuaja. Ninaamini hilo.

²¹⁰ Tazama ahadi za wakati huu. Lo jamani! Kila Nuru ambayo imeangaza... Hizi nyakati za kanisa tunaona jinsi... Li—limekuwa jambo la kuhuzunisha kuona kukataliwa. Ufunuo 3—nimeandika hapa chini Ufunuo 3, na ninajua kile—kile nilikuwa nakitaja wakati huo.

²¹¹ Tazama ahadi ya wakati huu, tunaishi, ni Nuru iliyokataliwa. Wao walifanya nini? Waliikataa kule nyuma. Kwa nini? Walikuwa wanaishi katika mng’aro. Wanafanya nini leo? Jambo lile lile. “Vema, wewe u—u Mkristo?”

“Mimi ni Mluteri!”

“Mimi ni Mbatisti!”

²¹² “Mimi ni Mpresbeteria.” Hilo halimaanishi kitu kwa Mungu. Hata afadhali ungesema u nguruwe mwitu, nguruwe, au cho chote upendacho kujiita. Waona? Hiyo—hiyo ndiyo maana yake. Sio—sio—sio kukudharau, bali ukilipeleka katika upande wa kimsingi, hiyo ni kweli. Ninauliza swali: Mkristo? Huyu ni Kristo ndani yako. Na kama Kristo yu ndani yako, basi Neno li ndani yako. Na kama—basi ikiwa Neno li ndani yako, wakati Nuru inaangaza, utatokaje nje yake? Waona, waona? Hilo ndilo swali. Hilo ndilo liko ndani sasa.

²¹³ Nuru, Nuru ya jioni inaangaza; Mti wa Bibi-arusi unachanua. Lo, kumbuka, waliupogoa huo Mti mzee. Na yaliyosazwa na parare, tunutu alikula; na yaliyosazwa na tunutu, madumadu amekula. Yaliyosazwa na Methodist, Batisti ilikula; na yaliyosazwa na Batisti, Pentekoste imekula. Alisema Mti huu (Yoeli) ulikatwa ukabaki shina tu, bali alitaka kujua kama ungeishi tena. Lo, ndio! Aliuhifadhi. Aliuhifadhi Mti huo (ndio, bwana!), kwa sababu ulikuwa Bibi-arusi Wake. Naye alisema, “Nitarudisha, asema Bwana.” Ni nini? “Nitayarudisha yote yaliyoliwa na Waluteri, yaliyoliwa na Wamethodisti, na hao wote. Nami nitayarudisha, kwani yote yangali katika mizizi ya ule Mti.” Unaona? Umelala kule katika ardhi, kama tu ule utomvu ulioteremka chini, kama nilivyosema kuhusu yule dada, umelala pale. Na baragamu ya Mungu itapigwa siku moja na hao Waluteri walioteuliwa, Wamethodisti, ambao hawakuhusika kamwe na dhehebu lolote...

²¹⁴ Luther hakuunda dhehebu lolote. Moody hakuunda dhehebu lolote. Ni kundi la akina Rickey waliokuja nyumaye waliounda dhehebu, wakachukua ganda. John Smith hakuunda dhehebu lolote. Hakuna mmoja wao aliyeunda dhehebu. Ilikuwa ni Nuru ya wakati ule. Luther, Wesley, au hakuna yeyote kati yao, ni lile kundi lililokuja baada yao lililounda dhehebu.

²¹⁵ Roho Mtakatifu hakuunda shirika lolote katika Pentekoste. Pentekoste ni tukio, sio dhehebu. Hakuunda dhehebu lolote. Lo, hash! Bali watu waliodai kuwa Wapentekoste waliunda dhehebu. Hilo ndilo ganda linalokufa kule. Badala ya kulifinyanga katika ile karatasi kuifanya sura kamili ya Yesu Kristo ijitokeze, la, wao walijiondoa nje. Basi hawana la kufanya ndani yake. Waacheni peke yao tu.

²¹⁶ Bali tunaona ya kuwa hii Nuru, mti huu...Kristo akikataliwa tena na kanisa. Kwa nini? Kwa sababu ile ile walimkataa kwanza, ile ming'aro bandia ya kale ya nuru za siku nyingine. Naye ni yeye yule jana, leo na hata milele; Waebrania 13:8 inasema ndivyo alivyo. Yeye yuko vivyo hivyo leo kama alivyokuwa wakati huo, kwa sababu anafanya jambo lile lile alilofanya. Neno lile lile ambalo Kristo...

²¹⁷ Sikiliza, nataka niwachukue sasa, na hebu hili liwe la kibinafsi. Sijui; sijaamua kabisa kama nitakizima hiki au la (mnaona) kwa ajili ya hicho chombo cha kunasa sauti. Nitakiacha kiendele.

²¹⁸ Ninataka kuwauliza jambo fulani. Tazama hili. Mnaona? Ni yeye yule jana, leo, na hata milele. Tazama, kazi Zake alizofanya zinajidhihirisha zenyewe. Sasa, sikilizeni kwa makini. Aliposimama pale katika Yohana 14:12, alisema, "Kazi nizifanyazo Mimi ninyi nanyi mtazifanya. Kubwa kuliko hizo mtazifanya, kwa kuwa Mimi naenda kwa Baba." Sasa, Yeye alisema hivyo. Mbingu na nchi zitapita, bali hilo Neno halitakosa kamwe. Sasa, kama tuko katika mwisho wa wakati huo, zile kazi kubwa zaidi zitakuja wapi? Mnaona, mnaona? Tuko hapa. Hatuna...

²¹⁹ Sikiliza, kama kalenda ya kirumi ni sahihi...Tuna—tuna miaka thelathini na sita iliyosalia. Kila miaka elfu mbili ulimwengu unakabiliwa na mwisho wake. Miaka elfu mbili ya kwanza ukaharibiwa na maji; miaka elfu mbili ya pili Kristo akaja. Huu ni wa 1964 unaokaribia, miaka thelathini na sita. Sasa, kalenda ya elimu ya nyota ya Kimisri yasema tuko nje miaka kumi na saba; iko miaka kumi na saba mbele ya hiyo. Hiyo inaacha miaka kumi na tisa iliyosalia. Yesu alisema kwamba hiyo kazi itafupishwa kwa ajili ya Wateule, la sivyo, hakuna wenye mwili watakaookoka. Tuko wapi? "Kazi nizifanyazo Mimi ninyi mtazifanya." Za aina ile ile, bali kubwa zaidi, mtazifanya.

²²⁰ Sasa tazameni. Sikilizeni kwa makini! Vaeni...Ninaomba kwamba Mungu atafungua moyo wako na akili yako upate kuelewa, ili uelewe bila kusema kuwa imezidi sana hapa. Angalia. Alisema siku moja...Hebu na tuone baadhi ya kazi kubwa alizozifanya. Hebu na tutulie tuone mambo kadhaa. Hebu na tufikiri. Wakati mmoja Yeye alisema, "Wapeni ninyi chakula."

Wakasema, "Hatuna kitu."

Kasema, “Mna nini? Nileteeni mliche nacho.”

Nao wakasema, “Tuna mikate mitano ya shairi na samaki wawili.”

²²¹ Akasema, “Nileteeni.” Kisha akaichukua ile mikate asili ya shairi akaanza kuimega hiyo mikate. Na kutoka ile ya asili, Yeye akafanya mikate na kuwalisha elfu tano. Hiyo ni kweli? Ndipo akasema, “Mna samaki? nileteeni samaki.” Mwanzoni ilikuwa samaki, na akatwaa kutoka ile samaki, samaki mwingine, na samaki mwingine, na kuwalisha elfu tano. Hiyo ni kweli? Bali katika siku ya mwisho Yeye hakuwa na kitu, Yeye alinena tu na kusema, “Sema itakuwapo!” na ilikuwa pale bila kuwa na kitu. Yeye hakuwa na kindi; hapakuwa na mmoja pale. Yeye alisema tu, “Wawepo!” wakawa! Lo, Neno Lake haliwezi kukosea. Lazima litimie.

²²² Ningewaambia mambo yanayoweza kuwatisha. Mnaona? Iko pale Yeye anaposema iko pale. Hebu Yeye na aseme hivyo. Mnaona? Sawa kabisa. Mnaona?

²²³ Waona, mashariki—magharibi hapa imerudi na kukutana na mashariki. Hata ni Musa aliyeokota changarawe akasema, “Na kuwe na chawa!” na kadhalika hivyo juu ya nchi. Lakini katika siku hii ya mwisho Yeye hachukui cho chote (mnaona?), ni Neno tu. “Na iwe, na ikawa.” Linalosemwa, hivyo ndivyo litakavyokuwa. Ninataka kutoa ushuhuda juu ya baadhi ya mambo hayo usiku huu (mnaona, mnaona?) juu ya yale yametendeka mpate kuona Yeye yuangali Mungu. Maneno Yake hayawezi... “Kazi hizi nizifanyazo, nanyi mtazifanya pia, na kubwa kuliko hizo mtazifanya. Nilichukua samaki kufanya samaki. Ninyi hata hamtahitaji kuwa na samaki.” Yeye yuangali Mungu. Yungali Mwana yule yule, Mwana yule yule wa Mungu aliyetoa samaki kwa samaki. Ni Mwana yule yule wa Mungu leo. “Kazi hizi nizifanyazo Mimi ninyi nanyi mtazifanya; hata kubwa kuliko hizo mtazifanya.” Zitazidishwa. “Kubwa zaidi ya hizi mtazifanya.” Na watu wanakataa kuliona. Kazi kubwa zaidi!

²²⁴ Nuru bandia! Unajua, nilikuwa nafikiria jambo fulani. Nilikuwa nikitaja sana kuhusu Uingereza, bali nilikuwa nikifikiria juu ya nuru bandia. Hapa sio muda mrefu uliopita, nyote mwakumbuka wakati ule wizi mkuu kabisa ambao—ambao umewahi kufanywa Uingereza. Huo ulifanywa na... Ulikuwa wizi wa dola milioni saba. Sidhani kumekuwa na mwingine duniani unaolingana na huo. Unyang’anyi mkuu, majuzi wa dola milioni saba. Hata Scotland Yard hawawezi kuuwazia. Mwajua walivyofaulu? Kwa nuru bandia. Waliwasha taa katika njia ya reli, hadhari, wakaendelea hata wakafikia kwenye taa nyekundu, ikawasimamisha, na pale wizi ukafanyika, katika mahali panapofaa. Nuru bandia ikawapa wizi mkuu sana ambao mataifa yamepata kuujuu.

Iliwaibia mataifa uvamisi mkubwa sana, unyang'anyi mkuu sana, ulifanywa kwa nuru bandia.

²²⁵ Na unyang'anyi mkuu sana ambao umepata kulikabili kanisa la Mungu ni nuru bandia, mng'aro wa dhehebu. Umewaibia nguvu za Roho Mtakatifu. Umeiondoa kanisani kamba ya kuokolea. Umewaibia Neno, walipokubali kanuni za imani badala ya Neno. Imewaibia...Lo, wanadai kuwa wana Neno. Neno hujiishia katika wakati wake, linajifanya lijulikane. Wanadai ya kwamba walikuwa na Neno pia kule nyuma katika siku za Yesu, lakini lilisema waliona Nuru kuu, nao wakaikataa. Waliiona, bali wakaikataa.

²²⁶ Lo, nuru bandia! Ndio, imeligharimu kanisa wizi mkuu kabisa uliowahi kuweko. Kanuni baridi za imani, ndugu, hazitaivisha Neno lililothibitishwa, la, punje moja, Biblia ilisema...Yesu alisema Neno la Mungu ni—ni Mbegu ambayo mpanzi hupanda. Mnaona? Na kanuni baridi hazitaivisha hilo Neno. La, La! Siku zenye baridi na upepo wa theluji hazitaivisha ngano. Hasha! Inahitaji joto la miali ya nuru ya jua, kwa sababu lilikuwa neno lililolenwa la Mungu kufanya jambo la namna hiyo. Na itahitaji Neno lililolenwa na Mungu leo kuonyesha watakatifu wa Mungu kuwa Yesu Kristo yu hai na vile alivyokuwa jana ndivyo alivyo leo. Kanuni za imani na madhehebu hayataweza kufanya hivyo. Hizo ni baridi na hazijali, na punje itaozea ardhini. Haiwezi kumea katika hali hiyo.

²²⁷ Hiyo ndiyo sababu ile—leo tuna yale tuliyo nayo. Kama ndugu wetu wa dhamani Billy Graham mfufuzi mkuu. Nafikiri Mungu anamtumia mtu huyo. Bali tazama anayofanya, anaenda kule miongoni mwa hao Wabatisti na Wapresbeteria. Anafanya nini? Anapata kundi la wajiunga na kanisa.

²²⁸ Mnaona pale Wabatisti wa Kusini wanavyojivuna sababu walikuwa na madhehebu mengi zaidi—dhehebu lao lilikua zaidi ya Waprotestanti wengine. Wakatoliki karibu wawachukue wote mwaka jana. Mnayaona gazetini? Walifanya hivyo kweli. Msifadhaika, itawachukua wote, kwa maana inachukua Wabatisti, na wote, wote pamoja. Na wote ni mmoja nao hawajui. Halmashauri ya—Halmashauri ya Makanisa inawafanya wote kitu kimoja. Madhehebu yanaweka...Mbona? Mbona utake kukaa hapa—humu? Mradi tu unakataa hili, kuna tofauti gani? Je, hamtumii kadi zilizo sawa za kidhehebu kama kwamba mko tu mahali pamoja, mmoja ni yule mnyama na mwingine ni ile alama, basi ndivyo hivyo. Kwa hiyo hakuna tofauti yoyote.

²²⁹ Ni pale alipokuwa. Ametia muhuri wake wa kibali, na pale mwauchukua. Na pale akaongoza mpaka Ikulu, mpaka Washington D.C. na—na ile Halmashauri ya Makanisa, na pale mwaenda! Makasisi waliwarudisha kule, sawasawa na vile

Biblia ilisema watafanya. Jamani, ningependa ile saa inge—haingeenda haraka hivyo.

²³⁰ Sasa, fikiria tu sasa mahali tulipo. Angalia ahadi za leo—zimekataliwa tena. Jinsi makanisa yalivyofanya katika siku hii ya mwisho, madhehebu.

²³¹ Mng'aro, kuishi katika mng'aro bandia ndio sababu haitaiva. Hiyo ndiyo sababu Neno hili—hamuoni miujiza.

²³² Kasisi fulani alinihoji si muda mrefu uliopita, akasema, “Bw. Branham,” akasema, “ulimbatizaje m—msichana fulani?” aliyetoka katika kanisa hili, naye akaanguka, na kuolewa na kijana Mkatoliki, na kuenda katika kanisa la Katoliki. Na yeye alikuwa ampeleka yule mwanamke kanisani.

²³³ Nikasema “Nilimbatiza katika ubatizo wa Kikristo.”

Akasema, “Askofu anataka kujua.”

Nikasema, “Vema, ndivyo ilivyo.”

Kasema, “Utaapa kwa hili?”

²³⁴ Nikasema, “Siapi kabisa.” Kisha akasema... Nikasema, “Ikiwa huwezi kuamini neno langu katika jambo hilo, hiyo ni sawa.” Nikasema, “Kama siapi... Biblia ilisema, ‘Msiape kwa mbingu; maana ni kiti cha enzi cha Mungu; dunia ndiyo ya kuwekea miguu Yake. Ndiyo yenu na iwe ndiyo na siyo, siyo.’” Nikasema, “Yakubidi uliamini neno langu.”

Kasema, “Vema, u—ulisema, ‘Ubatizo wa Kikristo,’ wamaanisha nini na hiyo, kwa kuzikwa majini?”

²³⁵ Nikasema, “Hiyo ndiyo njia ya pekee ya kufanya ubatizo wa Kikristo.” Nikasema, “Nilimbatiza katika mto Ohio, nilimzika majini katika Jina la Yesu Kristo na kumwinua tena. Nilimbatiza katika Jina la Bwana Yesu Kristo, ambao ndio ubatizo pekee wa Kikristo uliopo.”

Kasema, “Ndiyo bwana!” Akaliandika hivyo, na akasema, “Ajabu” kasema, “unajua, kanisa Katoliki lilikuwa likibatiza hivyo.”

Nikasema, “Lini?”

Na yeye akasema—kaendelea, na yale mazungumzo yakaendelea kwa muda, kisha akasema, “Vema, sisi ndio Wakatoliki wa asili.”

²³⁶ Nikijua pale, vilikuwa pale vi—vitabu, mnajua, na historia juu ya hilo, nikasema, “Hiyo ni kweli.” Bali nikasema, “Mbona hamfanyi hivyo leo?”

Akasema, “Tuna uwezo wa kuondoa dhambi.” Kasema, “Yesu... Si Yeye aliwaambia wanafunzi Wake, ‘wo wote mtakaowaondolea dhambi, wameondolewa; na wo wote mtakaowafungia dhambi, wamefungiwa?’”

Nikasema, “Ndiyo, bwana! Aliwaambia.”

Akasema, “Basi si hilo—basi si hilo hulipa kanisa mamlaka? Petro alikuwa kiongozi wa kanisa.”

²³⁷ Nikasema, “Kama kanisa litawaondolea dhambi vile Petro alifanya.” Nikasema, “Sasa, walipouliza, ‘Tufanye nini tupate kuokoka?’ Yeye alisema, ‘Tubuni kila mmoja wenu mkabatizwe kwa Jina Lake Yesu Kristo, mpate ondoleo la dhambi zenu.’” Nikasema, “Fanyeni hivyo, nami nitaambatana nanyi.”

“Lo,” akasema, “unajaribu kuitetea Biblia.”

Nikasema, “Hilo ni Neno.”

Akasema, “Mungu yuko katika kanisa Lake.”

Nikasema, “Mungu yuko katika Neno Lake. Neno la mtu mwingine ye yote ni uongo, Lake ndilo Kweli.” Mnaona?

²³⁸ Basi hakuna njia nyingine unayoweza kupata (waona?) ila hiyo. Pale wanaenda, wakiendelea gizani, na Wapentekoste kwa maelfu wakianguka ndani yake. Hapa wako katika kuzikubali kanuni zao za imani na mengineyo, wakiendelea moja kwa moja pamoja na... Na Neno likijitokeza na kulithibitisha, Yesu Kristo akijidhihirisha yeye yule jana, leo, na milele, na katika ule mng’aro wa kanuni za imani wanaendelea hata wakaingia gizani—katika giza, kama tu walivyofanya katika wakati wa Nuhu. Kama walivyofanya katika nyakati zote, wanafanya hivyo tena leo, katika giza hasa. Kwa nini? Wanakataa Nuru, kwa sababu kanuni zimewapofusha.

²³⁹ Lo, ni saa iliyotiwa giza kiasi gani tuliyo ndani yake Sasa. Naam, wanakataa Nuru ya Kristo ya kweli na ya milele, na hilo ndilo linafanya hayo.

²⁴⁰ Madhehebu baridi kamwe hayawezi kuleta Uzima kwa Neno la Mungu, kwa sababu linaleta uzima kwa dhehebu. Tuna wengi zaidi wanaokiri kuwa Wakristo sasa... Tazama hapa, kama Mkristo, nilimuuliza huyu kasisi hili: “Kama... Nitakubaliana nawe kwamba kanisa Katoliki mwanzoni lilikuwa katika Pentekoste, sio katika Nikea, Urumi.” Kanisa kamwe halikuanzia Nikea, Urumi; lilianzia katika Pentekoste. Mnaona? Pale Yerusalemu ndipo Kanisa lilianzia. Lakini nilisema, “Hapa, nitakubali kuwa watu hawa...”

²⁴¹ Wale watumwa na wengineo waliopokea Roho Mtakatifu, na mabwana zao wakaona uwezo wao na mengineyo, yale waliyokuwa wakifanya, kufufua wafu, kunena katika lugha, kutoa pepo, kutabiri mambo... Na manabii miongoni mwa, na kadhalika wakatoka wamevalia ngozi za kondoo, wakila majani, wakaja katika lile Baraza la Nikea na kadhalika... jinsi watu mashuhuri. Na pale wakatoka mle ndani, wakahudhuria lile Baraza la Nikea wakilitetea hilo Neno. Bali katika zile siku kumi na tano zenye umwagikaji wa damu, wao wakakubali Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu kama kanuni ya imani badala ya fundisho la Biblia katika Jina la Yesu Kristo. Kupitia hayo

makanisa yote ya Kiprotestanti yametokea, yamezaliwa katika hilo, jambo lile lile. Mambo haya mengine yote, kule kuelewa vibaya kwa Roho Mtakatifu. Walikuwa—wanachukua ushirika, kunywa divai, na hiyo ndiyo ushirika mtakatifu ambao maana yake ni Roho Mtakatifu. Kasisi anakupatia.

²⁴² Sasa, Biblia haimaanishi, “Hata ilipotimia siku ya Pentekoste, hapa yuaja kuhani barabarani, huku ukosi wake umegeuzwa, na kusema, “Toa ulimi wako upokee ushirika mtakatifu.” La! Haikusema, “Enyi watu wote njooni humu mbio mnipe mkono wa ushirika. Enyi Wabatisti, Wamethodisti, na Batisti, nitaliweka jina lako...Lete barua kutoka mahali fulani.”

²⁴³ Alisema wote walikuwa pamoja katika moyo mmoja, na kukaja ghafula toka mbinguni uvumi kama uvumi wa upepo wa nguvu ukienda kasi; ukakijaza chumba chote walichokuwa wameketi. Wote wakajazwa Roho Mtakatifu wakaanza kusema kwa lugha nyingine kama Roho alivyowajalia kutamka mle ndani. Wakatoka na kuingia barabarani, wakiymbayumba kama walevi, Mariamu na wengine wote, chini ya uwezo wa Roho Mtakatifu. Wakati watu walisema, wakawadhihaki na kusema, “Hawa watu wamelewa divai mpya!” walikuwa nini? Wamepofushwa na kanuni ya imani.

²⁴⁴ Yule muhubiri mdogo wa mbili kwa nne aliyesimama pale aitwaye Petro na, alisema, “Enyi watu wa Uyahudi na ninyi mkao—enyi watu wa Yerusalemu na ninyi mkao Uyahudi, lijueni jambo hili, mkasikilize maneno yangu. Hawa hawakulewa, bali hebu niwaambie vile Maandiko yalisema itakuwa. Hii ndiyo Nuru! Hii ni Neno likidhihirishwa!” Amina! Jambo hilo hilo latendeka leo, na wanafanya kama walivyofanya wakati ule, waliondoka wakitikiza vichwa vyao. Kasema, “Waacheni, kipofu akiwaongoza vipofu, wote wanaanguka shimoni.”

²⁴⁵ Lo, unahitaji Uzima wa Milele wa Kristo, kulileta Neno la Uzima lipate ku—kuthibitishwa. Kufanya mwili... Lo, jamani!

²⁴⁶ Yahitaji Neno la—yahitaji Roho Mtakatifu kulifanyiza kazi Neno la Mungu. Wakati Yesu alisema, “Enendeni ulimwenguni mwote, mkaihubiri Injili kwa kila kiumbe...” Sasa, tazama, Marko 16, agizo Lake la mwisho “ulimwenguni mwote—ulimwenguni mwote...” Haijafika huko bado. Mnaona? “...ulimwenguni mwote mkaihubiri Injili kwa kila kiumbe. Aaminiye (ulimwenguni mwote) na kubatizwa ataokoka; asiyeamini atahukumiwa. Na ishara hizi zitafuatana na hao waaminio... (“Watapeana mikono na...?” La! “Watakuwa washiriki wazuri wa kanisa?” La!) Kwa Jina Langu watatoa pepo. Watanena kwa lugha mpya. Watashika nyoka, au wakinywa vitu vya kufisha, havitawadhuru. Wakiweka mikono yao juu ya wagonjwa, watapata afya.” Lo jamani!

247 Mpaka wapi? Kila kiumbe. Kiasi gani? Ulimwenguni mwote mpaka atakaporudi tena. Ishara hizi. . . “Yeye aniaminiye Mimi, kazi nizifanyazo Mimi, yeye naye atazifanya. Hata kazi kubwa kuliko hizi atazifanya, kwa sababu ninaenda kwa Baba Yangu.” Lo, jinsi tunavyoweza kuyaondokea hayo ni zaidi ya niwezavyo kusema.

248 Tuko katika giza kuu zaidi sasa kuliko vile wao walivyokuwa. Sasa, nina vifungu kadhaa zaidi hapa kisha ningependa kufikia mwisho haraka niwezavyo. Tuko katika giza kuu zaidi kuliko walivyokuwemo. Ninajua ninawachosha hapa kwa zaidi ya saa moja na nusu, lakini mwaona, hii kanda inaendelea kule ndani. Mnaona, mnaona?

249 Wako katika giza kuu zaidi kuliko lile tulilomo. Nilitoa tamshi kwamba. . . Kwa nini? Mekanisa katika mng’aro huu ni madanganyifu mno, inaonekana kama ni kweli. Sasa, si Yesu alisema, Mathayo 24. . . Mathayo 24 Yesu alisema kwamba katika siku za mwisho zile roho mbili zitafanana sana mpaka ingewapoteza walio Wateule, kama yamkini. Kungekuwa na kundi teule litakalotoka na kufanya Kanisa katika siku za mwisho. Na haya madhehebu ambayo—ile wanayoita kweli yao itafanana sana na kile kitu halisi, hata itawapoteza walio Wateule, hata Wapentekoste.

250 Sasa mnajua, hautamchukua Mpentekoste na kumpoteza kwa fundisho la Kimethodisti au Kibatisti. Hautamwambia hivyo. Yeye anafahamu vizuri zaidi. Wala hautampoteza Mbatisti kwa fundisho la Kiluteri. Mnaona? Na wala hutaupokea Ujumbe—hautaupoteza Ujumbe sasa katika Neno hili kwa fundisho la Kipentekoste la Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu, na mambo haya yote hivyo na kule nyuma na mafundisho yote waliyo nayo katika ile taratibu ya kidhehebu. La, hata kidogo! Hautawapoteza kamwe, kwa sababu Wateule hawatapotezwa. La!

251 Ni nini? Ni nini? Kupoteza. Hii ming’aro, inafanya nini? Inaliongoza kanisa kwenye machijio ya lile baraza kwa mng’aro wao. Huku kutakuwa kuchinjwa kwa mwisho wakati hilo pamoja na Urumi watakapopatana. Watakapofanya ile chapa ya mnyama, huko ndiko kuchinjwa kwa mwisho. Na hii ming’aro mliyo nayo sasa, tazama yale inafanya. Kuwaongoza watu. Ni mbuzi.

252 Mbuzi daima huwaongoza kondoo machinjioni. Mmeona hayo katika vibanda vya kuchinjia. Mbuzi atakimbia pale juu na kuwaongoza kondoo, halafu ataruka kando na kuwaacha kondoo waendeleo wakatumbukie. Mnaona? Hivyo ndivyo anavyofanya. Hufanya hivyo daima. Mbuzi ndio waliomwongoza Yesu, Mwana-Kondoo, mpaka machinjioni, mbuzi wa Kirumi. Hiyo ni kweli! Ni—ni mbuzi wa kidhehebu leo ndio wanaowaongoza kondoo wasio na hatia mpaka

machinjioni. Wanajiweka—majina yao katika vile vitabu kule na wamekwisha. Hiyo ndiyo chapa ya mnyama. Nanena katika Jina la Bwana. Nimeshikilia hilo kwa muda mrefu; hiyo ni kweli. Hiyo ni sawa kabisa! Mnyama ni nini? Mnyama ni nini? Ni utawala wa kidini wa Kirumi, dhehebu la kwanza. Chapa yake ni nini? Jambo lile lile. Sawa kabisa! Jambo lile lile hasa hilo lililokuwa. Machinjioni . . . Mpaka ule mng'aro . . .

²⁵³ Lakini usoni pa giza ya sasa bado tumeona Nuru ya Mungu ikiangaza. Jinsi tunavyoshukuru kwa hayo!

²⁵⁴ Sikilizeni kwa makini! Tumeiona Nuru, Neno Lake aliloliahidi kwa siku hii likithibitishwa na kuhakikishwa (ni kweli); Nuru ya saa hii. Lo, Jamani! Nina furaha sana. Hakuna kasoro yo yote. Kuna . . .

²⁵⁵ Hapa si muda mrefu uliopita muhudumu alikuwa akisema kuwa alikuwa kule Florida, na alikuwa na—na gari (naamini lilikuwa la aina ya Chevrolet), na likaharibika. Hakuweza kulitengeneza. Akaenda kwenye gereji; na maskini fundi mzee alikuwa akienda chini yake, na juu yake, na kuligusagusa, hakuweza kulitengeneza. Naye a—angejaribu hiki, na haikufaa kitu. Na angejaribu kingine; hakikufaa kitu. Aliweka jenereta, akaweka *hiki*, akaweka pulaki, akaweka pointi; hakuweza kukitengeneza kitu hicho kifanye kazi. Hakuweza kukitengeneza. Mwishowe mtu aliyevalia vizuri akajitokeza; akasema, “Naweza kukushauri?”

²⁵⁶ Yule fundi mdogo alikuwa na akili ya kutosha kusema, “Ndiyo, bwana!” Akasema, “Chukua *hiki*, na mara *hiki* na *hiki* na,” kasema, “weka hizo pamoja mara moja na ulijaribu.” Naye akachukua *hiki* mara *kile* na kuviweka pamoja, na pale likaanza kwenda.

²⁵⁷ Yule fundi mdogo akageuka na kusema, “Aisee, wewe ni nani?” Alikuwa mhandisi, mhandisi mkuu wa General Motors. Ndiye aliyelitengeneza gari hilo. Ndiye aliyelibuni.

²⁵⁸ Na leo tunapozungumza kuhusu Methodisti, Batisti, na Presbeteria, yule Fundi Mkuu yu hapa, Mbuni wa Neno Lake, yule Mtu aliyeumba mbingu na nchi na kulibuni Kanisa Lake. Ni Yeye ajuaye zaidi yale yanayohitajika kwa kunyakuliwa au ni kanisa la Mmethodisti au Kibatisti linalojua zaidi yale yanayohitajika? Yeye ndiye Mbuni; Yeye anajua yanayohitajika. Yeye amevalia sawasawa katika uwezo wa kufufuka Kwake. Haleluya! Anatembea miongoni mwetu leo katika uwezo wa kufufuka Kwake. Anajua yanayohitajika kuliweka Kanisa katika hali ya kunyakuliwa. Alilibuni na kuziweka sehemu hizo pamoja hapa katika Biblia. Amina! Acha mkondo wa nguvu za spaki upitie ndani yake, sasa itazame ikifanya kazi. Iache imani katika Neno Lake lililoahidiwa la leo ipitie ndani yake, utaona vile linafanya kazi. Kwa nini? Alikibuni kitu hicho. Yeye alilibuni Kanisa Lake kwa Neno. Hilo ndilo aliweka pamoja, si

kwa dhehebu la Kimethodisti, au Kibatisti, au Kipresbeteria, wala Kipentekoste, bali kwa Neno Lake. “Mtu hataishi kwa mkate tu bali kwa kila Neno litokalo katika kinywa cha Mungu.” Ndiyo, bwana! Ondoka katika hiyo ming’aro!

²⁵⁹ Katikati ya giza, wakati huu wa giza tunaishi ndani yake sasa. . . Nina kama dakika tano tu zilizosalia. Katikati ya giza ni nani atakayemtoa nje Bibi-arusi mdogo. Ni nani ajuaye jambo hilo? Yule Mbuni Mkuu. Lo, ndivyo! Kutoka hali hii yote ya kutatanisha ya mng’aro. . . Hapa Wamethodisti wanang’ara upande mmoja, Wabatisti mwingine, na Wapresbeteria mwingine na Wapentekoste mwingine, ming’aro hii yote hapa. . . Wanakimbia, wanaweka jina lao hapa katika mng’aro huu. Naam, kuja kutambua jambo fulani pale, na kuja hapa, na jambo fulani pale, kuja humu. . .

²⁶⁰ Kama nilivyomwambia yule kasisi, “Ikiwa nyote ni kanisa la asili na mlifuata fundisho la watu hawa waliokutana Nikea, mbona hamna uwezo waliokuwa nao kule nyuma katika mwanzo basi? Mbona hamfanyi yale waliyoyafanya, ambayo Yesu alisema. . .”

Kasema, “Lo, tu watu wengi zaidi leo; sisi—sisi tunaishi katika wakati tofauti.”

²⁶¹ Nikasema, “Lakini Neno halibadiliki. Yeye alisema, ‘Ishara hizi zitafuatana nao kwa nyakati zote. Mbingu na nchi zitapita, bali Neno Langu halitapita kamwe.” Ndiyo hiyo!

Akasema, “Unanena kuhusu Biblia.”

²⁶² Nikasema, “Ndiyo, lile Neno ambalo ni Kristo.” Hiyo ni kweli. Na basi hivyo ndivyo ilivyo. Waona?

²⁶³ Na katika mng’aro huu, Wamethodisti wakionyesha wao, Wabatisti wakionyesha wao, Wapresbeteria wao, kila moja likiendelea kukua kuwa kubwa zaidi na zaidi wakati wote, maskini Bibi-arusi mdogo, yuko wapi? Alienda hapa kwa Wapentekoste wa umoja kwa muda, akaweka jina lake pale, naye angesema, “Vema, naja kuona yale wanayofanya.” Wanakuja huku, na, “Lazima uwe mshiriki wetu. Kama wewe si mshiriki wa kanisa letu, wewe hata hauko katika Bibi-arusi. Hata hu kitu.” Kaenda hapa kwa Assemblies, na angalia yale waliyo nayo. Ndivyo ilivyo tena. Kaenda kwa Wabatisti, angalia waliyo nayo. Tazama yale. . .

²⁶⁴ Itakuwaje kwa yule maskini mdogo. Mnaona? Lakini Yeye atajitokeza; usifadhaike. Yeye atakuwepo pale.

²⁶⁵ Mtu fulani alikuwa akisema hapa yapata miaka kadhaa iliyopita, alikuwa kule New Mexico. Nilifanya mkutano pale karibu na Mapango ya Carlsbad. Mmesikia juu yao kule chini, yale makuu. . . Nao wakamchukua mtu, na mkewe, na kundi la watoto, wakaenda katika lifti wakateremka kwenye kina cha shimo. Na walipofika kule chini, wakazima taa zote.

Na walipozima taa zote, ikawa giza ya usiku wa manane. (Walimfanyia hivyo hapa katika bustani hizi hapa katika—na wakati mmoja katika—kule Colorado pale, mimi na mke wangu, pale nyuma, tulikuwa mle ndani. Nao wakaziwasha zile taa—jamani, unaweka mkono wako hivi, hungeona kitu.) Na palikuwepo msichana mdogo amesimama pale, akaanza kupiga mayowe, “Lo!” akapiga mayowe. Alikuwa—alikuwa ameogopa mno kulikuwa giza sana. Maskini mtoto yule alikuwa akipapasa kila mahali na kujaribu kupiga mayowe na kumlilia baba yake, mama yake kila mahali. Hangelivumilia, kulikuwa giza kuu. Hakuwa ameona giza kama hilo.

²⁶⁶ Na karibu ndivyo ilivyo sasa. Hiyo ni kweli! Kuna giza sana hujui pa kuenda. Unaenda kwa Methodisti, unaenda kwa Batisti, unaenda kwa Presbeteria, yote ni kitu kile kile. Unaona? Wanakula ile mana ya kale, iliyoza, iliyo na wafurukuta mikia. Waona, jambo lile lile, fundisho fulani, “Ingia ujiunge na *hili*, jiunge na *lile*,” fundisho la kale na kila kitu, haumwoni Kristo ndani yake. Lo, unaona watu wanaojiona kuwa na haki na mengineyo. Wengi ni watu wazuri mle ndani sasa, katika hayo madhehebu. Ninasema lile dhehebu, sio watu walio humo. Lakini unaona, hayo ndiyo wanayokula. Waambie kuhusu hilo. Hapa kuna Chakula safi!

²⁶⁷ Na huyu msichana mdogo akisimama pale, anapiga mayowe kwa sauti yake yote, nusura apatwe na wazimu, karibu vile Bibi-arusi mdogo alivyo. Lakini wajuaje, ndugu yake mdogo alipaza sauti, akasema, “Dada mdogo, usiogope (kwa sababu alikuwa amesimama karibu na mhandisi!)” Kasema, “Yupo mtu hapa anayeweza kuiwasha taa.” Usiogope, Dada mdogo, kuna Mtu hapa anayeweza kuiwasha Taa. Anaweza kulifanya Neno hili liishi. Hatujui atakavyokuja—hatujui jinsi—wakati atakapokuja; sijui lo lote kuhusu hayo, bali Yuko hapa. Na anaweza kuziwasha Taa. Tutatokaje nje yake? Sijui, bali Yupo hapa, na ndiye awezaye kuziwasha Taa. Ndiyo bwana! Ndiye; Yeye ndiye Nuru. Yeye anajijulisha Mwenyewe tu; hivyo ndivyo anavyoiwasha Taa. Sawa kabisa. Inahitaji Kristo kuziangaza Nuru Zake, na ndipo giza lote linatawanyika. Yeye anatenganisha; Yeye anamvuta Bibi-arusi Wake mdogo atoke. “Nitawatoa watu kutoka Mataifa kwa ajili ya Jina Langu, watakaokuwa na Jina Langu.” Jina Lake ni nani? Vema! Sio Methodisti, Batisti, Luteri—Yesu Kristo. Hiyo ni kweli!

²⁶⁸ Yeye ndiye Nuru, kweli, Nuru. Na hamna giza ndani Yake. Na Yeye hutawanya giza aingiapo, kwa sababu Yeye ni Neno. Neno ndilo Nuru. Hiyo ni kweli. Kwa sababu alinena na kusema, “Iwe nuru!” hilo ndilo Neno lililofanyika nuru. Anaposema hili, ndiyo Nuru ya wakati ule kila mara. Sasa, Yeye yuko humu ndani katika—katika, sio katika mng’aro, bali (watu wakiishi katika mng’aro), lakini Yeye ni Neno lililothibitishwa. Yeye kabisa ni— hiyo Nuru katika wakati wa giza. Ndiyo, bwana!

Hii ming'aro yote na kadhalika ya bandia itakwisha. Ndiyo, bwana! Yeye yuko hapa. Usiogope! Washa hizo Taa, Neno Lake lililoahidiwa, liko hai; linafanya . . . “Yeye aniaminiye Mimi, kazi nizifanyazo . . . yeye naye atazifanya.” Basi ni Neno. “Kama Baba alivyonipeleka, nami ninawapeleka.” Baba aliyempeleka Yeye, alikuja ndani Yake. Yesu anayekupeleka, anakuja ndani yako. Na kazi alizozifanya wakati huo, anafanya vivyo hivyo, kwa nini? Neno linafanyika mwili, katika mwili wa mwanadamu, likijidhihirisha kama Nuru ya siku hii. Haya basi. Liko pale, liko tu kama—kuonyesha njia ya Uzimani katika Nuru.

²⁶⁹ Watu wenye hekima ambao hawajapofushwa na kanuni za imani na dhehebu watatembea katika hiyo Nuru. Lo jamani! Yupo mtu hapa awezaye kuziwasha Taa basi. Yeye anafanya nini? Kwa kulithibitisha Neno Lake la siku hii. Yesu Mwana wa Mungu, aliyeahidi Neno kwa siku hii, yuko papa hapa pamoja nasi. Usiogope; sijali yale wanayofanya. Ukijali, utatembea katika giza. Iweni na hekima! “Wao watakaokuwa na hekima,” Danieli alisema, “katika siku hizi za mwisho watatenda mambo makuu kwa Mungu wao.” Mnaona, waona? Watatembea katika Nuru kama vile Yeye alivyo katika Nuru.

²⁷⁰ Usifadhaike; huenda ikawa giza, yaonekana kwamba watatulazimisha kila mmoja wetu . . . Haya yote . . . Unaona tangazo likitolewa, haya makanisa madogo yote na mengineyo yana—lazima yaingie ndani sasa. Lazima muingie ndani, au watawafungieni. Watafaulu.

²⁷¹ Sasa, tungependa kutilia hilo mkazo sana usiku wa leo, nitakapofikia wakati huu. Mnaona?

²⁷² Sasa, tutamaliza. Lazima uwe mmoja wao au la. LItakuwa—utakuwa ndani ya hayo au huwezi kufanya lo lote, hata huwezi kununua wala kuuza. Ndio bwana! Usidhubutu kuwaombea wagonjwa. Ukipatikana unamhudumia mgonjwa ye yote au mtu ye yote aliye na jambo la kiroho mle ndani, unaweza kushitakiwa chini ya sheria ya nchi ukauawe. Hiyo ni kweli kabisa. Mnajua hivyo. Hiyo ni kweli, iko magazetini mwao. Ndiyo, bwana! Basi huwezi kufanya hivyo. Lazima uwe mshiriki wa kundi hilo. Ndugu, hebu nikwambie jambo fulani, ni heri umwingize Kristo hapa moyoni mwako sasa hivi, kwa sababu wakati waja ambapo utahitaji hilo sana. Hautakuwa wakati huo. Kumbuka, wakati ule muhuri utakapotiwa, utakuwa humo milele. Basi usifanye hivyo, usiamini mambo hayo. Wewe ingia katika Kristo kabisa sasa, lile Neno.

²⁷³ Ndiyo, bwana! Hulithibitisha lile Neno na kuonyesha kwamba Ndiyo Nuru ya saa hii. Hivyo ndivyo tunavyojua kuwa Yeye ndiye Nuru, kwa sababu Yeye ni Nuru ikijidhihirisha katika mwili. Twajuaje? Alikuwa Neno la Mungu lililofanyika mwili. Mnaona? Neno la Mungu lilikuwa likijionyesha lenyewe akijidhihirisha Mwenyewe.

274 Masihi atakapokuja, yale atakayofanya. Mwanamke yule kisimani, alisema, “Masihi atakapokuja atafanya mambo haya. Lazima uwe yule Nabii, ambaye ni Neno, ukitutabiria mambo haya.”

275 Akasema, “Mimi ndiye!” Mnaona? Hiyo ilitosha. Nuru lililiangazia Neno lililoahidiwa. Kuna Nuru.

276 Akaenda moja kwa moja mjini, akasema, “Njooni, mtazame mtu aliyeniambia mambo yote niliyotenda. Je! haimkini huyu kuwa ndiye Masihi?” Hiyo ilikuwa kweli, Waona? Si hoja wengine walisema nini, Yeye alijua huyo alikuwa Masihi.

277 Kumbuka, katika kila wakati wa giza Mungu daima amekuwa na Neno Lake la kutenganisha Nuru na giza. Alikuwa nalo katika siku za Luther wakati kanisa Katoliki lilikuwa na kila kitu. Alimpeleka Luther kama Nuru iangazayo. Naye Luther akatenganisha Kweli na giza. Na wakati Waluteri walipotatanishwa, akamtayarisha John Wesley. Naye akatenganisha Nuru na giza. Na katika siku za Pentekoste wakati Wamethodisti walipo—nao Wamethodisti walipojitatanisha, na Batisti, na Presbeteria, aliupeleka ujumbe wa Pentekoste kutenganisha Nuru na giza. Pentekoste ikarudi tena mpaka gizani vivyo hivyo tena katika dhehebu lao, ikachukua kanuni zao za imani na mengineyo. Sasa, saa imewadia ambapo Neno hili litathibitishwa. Anapeleka Nuru, Neno lililodhihirishwa, kama alivyofanya mwanzoni, anapeleka Neno, na linajithibitisha Lenyewe. Kuna Nuru. Naye daima hutenganisha. Nayo hiyo leo ndiyo Uzima wa Milele kama ilivyokuwa hapo mwanzo.

278 Mkitazama, enyi watoto . . . Kama ninavyosema, nimepitisha muda kwa dakika tano sasa, lakini hebu niseme neno hili moja. Kuna Mtu aliyepo; usiogope hata waseme nini. Nimeona ikifikia kiwango ambapo sikujua mahali pa kuenda tena. Lakini Yeye daima yupo. Uwepo usiokosa, Yeye daima yupo. Anaweza kuiwasha Taa. Ndiyo, bwana! Yeye anangoja tu, aone yale atakayofanya. Anaweza kuibonyeza swichi wakati wo wote appendapo. Ndiyo, bwana!

279 Yupo Mtu hapa anayeweza kuiwasha Taa. Na watu waliokaa katika nchi ya uvuli wa mauti, wengine wao chini ya kansa, wengine wao katika mauti ya dhehebu, wengine wao chini ya mauti ya kanuni za imani, wengine wao chini ya mauti ya mapokeo, na namna zote za mauti, nao wameona Nuru kuu. Yule Mtu aliyeiwasha Taa wakati huo, ndiye yule yule aliyesema mwanzoni, “Iwe Nuru!” Mungu yule yule jana, leo, na hata milele, Yeye yupo leo, papa hapa sasa. Msiogope; anaweza kuziwasha Taa. Mateso yanapokuja, usiogope; kuna Nuru iliyosema atawanyakua watu wake. Bibi-arusi hataingia katika ile dhiki. Hatapitia mle kamwe. Yeye alisema hatapitia katika hiyo. Atanyakuliwa. “Watafanyaje hivyo, Ndugu Branham,

inaonekana kuna giza kuu sana?” Hata iwe giza namna gani, kama huwezi kuuona mkono wako mbele yako, kumbuka tu, yupo Mtu hapa anayeweza kuiwasha Taa, anaweza kulinyakua lile Kanisa.

²⁸⁰ Unasema, “Naam, niko ndani...” Ndiyo, Shadraka, Meshaki na Abednego walikuwa ndani kabisa mwa ile tanuru iliyowaka moto, bali kuna mtu mle ambaye anaweza kufungulia hewa. Ndiyo, bwana! Huo upepo ulioenda kasi, upepo wa nguvu ulioshuka chini siku ya Pentekoste, aliufungulia tena na kupuliza miali yote iwaondokee, moto wote. Kulikuwa na Mtu pale; Yeye anaitwa Mtu wa Nne. Kuna Mtu hapa leo, ndiye wa Pekee! Halleluya! Ana swichi ya kuwasha taa mkononi Mwake.

²⁸¹ Na wale walio katika nchi ya uvuli wa mauti, Nuru kuu iliwazukia. Usiikatae; ipokee katika Jina la Bwana, tunapoinamisha vichwa vyetu kwa muda mfupi.

Tutatembea Nuruni!
 Nuru nzuri!
 Njoooni ambapo matone ya umande wa rehema
 yanang'ara.
 Angaza kutuzunguka mchana na usiku,
 Yesu, Nuru ya ulimwengu.
 Tutatembea Nuruni!
 Ni Nuru nzuri sana!
 Huja ambapo matone ya umande wa rehema
 yanang'ara.
 Angaza kutuzunguka mchana na usiku,
 Yesu, Nuru ya ulimwengu.
 Njoooni, enyi watakatifu wa Nuru, tangazeni
 Yesu, Nuru ya ulimwengu.
 Ndipo kengele ya Mbinguni italia;
 Yesu, Nuru (Ni nini? Neno lililodhihirishwa ni
 Yesu leo; Yeye ndiye Neno).

Tutatembea Nuruni!
 Ni Nuru nzuri sana!
 Huja ambapo matone ya umande wa rehema
 yanang'ara.
 Lo! angaza kutuzunguka mchana na usiku,
 Yesu, Nuru, ya ulimwengu.

²⁸² Huku mmeinamisha vichwa vyenu nashangaa ni wangapi hapa wangependa kutembea katika Nuru hii chini ya uongozi wa Roho Mtakatifu, Neno lililodhihirishwa la siku hizi (waona?) Neno ambalo Mungu aliliahidi kwa siku hii, kuliona likidhihirishwa? Si hivyo ndivyo alivyokuwa hapo mwanzo? Alikuwa Neno. Mwana akazaliwa; alikuwa Neno; alikuwa Masihi; alikuwa Neno lililothibitishwa. Basi lile Neno... Mungu alinena mwi—mwisho tokea mwanzo.

²⁸³ Sasa, kuna Neno kwa ajili ya siku hii, na Yeye yuko hapa akilithibitisha hilo Neno katikati ya machafuko, giza, na ming'aro. Laonekana sana kama hilo, bali silo; halithibitishi kuwa ndilo. Mtafuta makosa . . .

²⁸⁴ Yesu alisema, “Ikiwa ninatoa pepo kwa kidole cha Mungu, na nyinyi je, huwatoa kwa nani?” Hawakuwatoa. Mwaona? “Lakini sivyo, ikiwa natoa pepo kwa kidole cha Mungu, basi Ufalme wa Mungu umekwisha kuwajilia.” Mnaona? Lo, hebu na tufikirie hilo tunapoinua mikono yetu pole pole sasa na kutafakari kwa utulivu sana.

Tutatembea katika Nuru hii!

Hii ni Nuru nzuri sana!

Na huja ambapo matone ya umande wa rehema yanang'ara. (Fanya maungamo yako; mwaamini Mungu sasa.)

Angaza kutuzunguka mchana na usiku, Yesu, Nuru ya ulimwengu.

Tutatembea katika Nuru hii!

Ni Nuru nzuri sana!

Huja ambapo matone ya umande wa rehema yanang'ara.

Angaza kutuzunguka mchana na usiku, Yesu, Nuru ya ulimwengu.

²⁸⁵ Wanapoendelea kuucheza wimbo huo, ninataka kuuliza . . . Kila wakati umekuwa vivyo hivyo. Katika siku za Nuhu wale waliokataa ile Nuru, walifanya nini? Waliingia katika hukumu ya Mungu. Nini kilitendeka kwa Farao katika siku za Nuru ya kile kijiti kilichowaka moto kilichokuwa katika Musa? Waliingia katika bahari ya mauti. Nini kilitendeka kwa Dathani aliyeanza halafu akaikataa Nuru? Aliingia katika ufa wa nchi uliomumeza. Nini kilitendeka katika nyakati zote kwa wale walioshindwa kutembea katika Nuru, Nuru ya siku hiyo? Ni Yesu wakati wote. Ilikuwa ni Yesu katika siku za hao watu. Ni Yesu leo, kwa maana Yeye ni Neno, na Neno hufanya ile Nuru. Ni Nuru ya siku hii. Litafakari sasa kwa utulivu tunapo—kwa unyofu wote tunapouliza, “Unatembea katika Nuru?” Tunapouvumisha wimbo huo tena . . .

[Ndugu Branham anaanza kuuvumisha wimbo—Mh.]

Nuru nzuri!

Huja ambapo matone ya umande wa rehema yanang'ara.

Angaza kutuzunguka mchana na usiku, Ee, Yesu, Nuru ya ulimwengu.

²⁸⁶ Hebu sasa tusimameni kwa miguu yetu. Ninamwomba Baba wa mbinguni auruhusu ujumbe huu ukolee vilindini mwa mioyo ya watu walio hapa na wale watakaosikia kwenye kanda. Na

hebu ile Nuru ilizukie lile Neno, ile mbegu, na kuotesha kila mbegu iliyoteuliwa iliyopandwa hapa nje katika hii ming'aro na madhehebu mbalimbali. Hebu waone kama Nikodemu, hata ikiwa itawabidi waje usiku. Njoooni kwenye Nuru! Tujalie, Baba.

²⁸⁷ Hebu lijitokeze jambo hili kuu la mwamba uliokatwa mlimani pasipo kazi ya mikono. Utazivunja hizi falme za Mataifa na kuziangamiza, falme hizi zote, falme za kiroho na za kawaida, na ule Mwamba utafunika dunia yote; itakuwa kazi ya utakaso. Wale watakaosagwa na huo Mwamba watakuwa kama unga, wale watakaoanguka juu ya huo Mwamba watakuwa na msingi imara.

²⁸⁸ Ee, Kristo, niruhusu mimi kama mtumishi Wako nifie juu ya huu Mwamba, huu mwamba wa Neno Lako. Bwana Mungu, niruhusu nisimame kama Daudi na wale askari wa kale waliomtetea Daudi. Niruhusu nilitetea hili Neno leo nionapo limekataliwa na madhehebu. Limelala juu mahali padogo pa salama. Ee Mungu, nina—tujalie tuwe na nguvu na ushujaa na Roho Mtakatifu tuweze kusimama, kwa maana majira haya yanaendelea kuwa na giza zaidi na zaidi. Lakini hebu nasi daima tukumbuke kwamba Wewe upo kuwasha Taa wakati wo wote upendapo. Unaweza kuiwasha Taa, Baba.

²⁸⁹ Kwa hivyo tunaomba, kama Wewe ulivyosema, “Ninyi ni Nuru ya ulimwengu.” Tujalie Bwana, ili Taa zetu—sisi tunaokutumikia—zikaangaze sana kwa wengine, wapate kuiona Nuru ya Injili tunapoiishia, Bwana, siku baada ya siku, tukiwaonyesha Maisha ya Yesu Kristo jinsi alivyokuwa duniani, mwingi wa unyenyekevu na Wema, hata hivyo akiwa Neno lililoishi ndani Yake. Tujalie, Bwana, kwani twakutazamia Wewe, uliye Mkuu na mwenye swichi mkononi Mwako. Wewe unaushika ulimwengu mkononi Mwako; unashika vitu vyote mkononi Mwako, na kuutegemeza ulimwengu Kwa Neno Lako. Ee Baba, hebu tulipokee Neno, tafadhali, Bwana. Ruhusu huo uwe ushuhuda, na shauku ya kila moyo hapa.

²⁹⁰ Na Baba, tunapoimba nyimbo hizi...Kama Daudi alivyoimba nyimbo, zikawa unabii. Zilikuwa unabii, na Wewe ukazitambua kuwa unabii. Tunapouimba, Bwana, ruhuru iwe hivyo katika moyo yetu pia tunapoimba *Tutatembea katika Nuru hii*. Na iwe hivyo, Bwana. Hii ni Nuru nzuri, ni Neno, ni Kristo akiishi miongoni mwetu, si vile alivyokuwa, vile alivyo. Nasi tunajua jinsi alivyokuwa ilionyesha tu jinsi Yeye alivyo. Basi tunaomba, Baba, kwamba watu wataelewa na kutembea katika hii Nuru nzuri. Tunaomba katika Jina la Yesu.

²⁹¹ Na tunapoendelea kusimama kwa muda mfupi, ningependa sote tuimbe.

²⁹² Sasa, humu ndani kuna Mpresbeteria, Methodisti, Mkatoliki, hili ni kundi lililochanganyika tukinena kidhehebu.

²⁹³ Sasa kumbuka, na ijulikane kwamba sisemi cho chote dhidi ya watu walio katika hii ming'aro, bali nimeithibitisha kwa Biblia kuwa ni ming'aro. La, sivyo, Kristo angekuwa anafanya vile aliahidi kufanya pamoja nao. Mnaona? Bali wamekataa hayo. Mnaona? Na unapofika pale, unapata nini? Kujiunga na kanisa, kukariri kanuni za imani. Bali matokeo yake ni nini. Ukifika mwisho wa safari yako, unatambua ilikuwa mazigazi bandia. Kristo ni Neno; Yeye ndiye Nuru. Ishi sasa uwezapo kuishi.

²⁹⁴ Unaishi kwa ajili ya jambo fulani. Kwa nini unaishi? Ili upate kufa. Kila mmoja wenu, kwa nini unafanya kazi? Upate kula. Kwa nini unakula? Ili uishi. Kwa nini unaishi? Ili ufe. Mbona basi usiishi upate kuishi! Mbona usiishi upate kuishi! Ndipo njia pekee uwezayo kuishi ni kulikubali Neno, "Kwa maana mtu hawezi kuishi kwa mkate tu (yale tunayopata hapa kwa jasho la uso wetu), ila kwa kila neno litokalo katika kinywa cha Mungu." Sasa, Neno la kinywa cha Mungu linathibitishwa papa hapa mbele yetu na Roho Mtakatifu. Ishi kwa Hilo, sivyo?

²⁹⁵ Sasa, ningependa tunapouimba huu tena, hebu kila mmoja wetu asimame tu mahali petu, anyoshe mkono na kuushika mkono wa mtu mwingine na kusema, "Ndugu, hebu na tutembe katika hii Nuru!" tunapoimba "*Tembea Nuruni*," mtafanya hivyo? Ombeaneni mnapoweka mikono yenu pamoja, tunapouimba pamoja, tukifunga macho yetu tuwezavyo.

Tutatembea Nuruni!
Ni Nuru nzuri!
Inakuja ambapo matone ya umande wa
rehema yanang'ara.
Angaza kutuzunguka mchana na usiku,
(Ni nani?)
Yesu, Nuru ya ulimwengu

Sasa, hebu tuinue mikono yetu!

Tutatembea Nuruni!
Ni Nuru nzuri!
Inakuja ambapo matone ya umande wa rehema
yanang'ara
Angaza kutuzunguka mchana na usiku.
Yesu, Nuru ya ulimwengu.

Njoooni enyi watakatifu wa Nuru, tangazeni (Ni
nini?)
Yesu Nuru ya ulimwengu.
Ndipo kengele za Mbinguni zitalia,
Yesu, Nuru ya ulimwengu.

Lo, hebu tuuimbe kabisa sasa.

Tutatembea Nuruni!
 Ni Nuru nzuri!
 Huja ambapo matone ya umande wa rehema
 yanang 'ara.
 Angaza kutuzunguka mchana na usiku,
 Yesu, Nuru ya ulimwengu.

²⁹⁶ Huku vichwa vyetu vimeinamishwa sasa, kumbukeni, Israeli walipokuwa safarini wakila mana mpya kila siku, wao walitembea katika Nuru ya Nguzo ya Moto. Hiyo Nguzo ya Moto ilikuwa Yesu Kristo. Biblia inasema ndivyo ilivyokuwa. Na leo Yeye yu pamoja nasi. Tunayo; tunajua Yeye yu pamoja nasi, Nguzo ile ile ya Moto, akitenda mambo yale yale aliyotenda alipokuwa hapa duniani kutimiza Neno Lake.

²⁹⁷ Tunapotoka hapa, hebu tukumbuke, tuweke wimbo huo mioyoni mwetu tunapoenda manyumbani mwetu, magurudumu yanapouvumisha wimbo. Kabla hujakula chakula chako cha jioni, inamisha kichwa chako umshukuru Mungu kwa kutuma nuru kuleta chakula duniani kwa mwili wako wa kawaida. Halafu mshukuru Mungu kwa kutuma Nuru ya Kiroho, Neno Lake, apate kuipa nafsi chakula, "Kwa maana mtu hataishi kwa mkate tu, ila kwa kila neno litokalo katika kinywa cha Mungu."

²⁹⁸ Endeeleni kujiimbieni wimbo huu nyumbani mwenu, miongoni mwa watu wenu, na mkutane nasi hapa tena yapata saa 12:30 jioni kwa ajili ya kadi za maombi na kadhalika. Tutawaoneni wakati huo. Mpaka wakati huo, inamisheni vichwa vyenu. Nitamwuliza Ndugu Neville kama atakuja hapa sasa, mchungaji, na kuturuhusu tuondoke kwa maombi mafupi. 

YUPO MTU HAPA ANAYEWEZA KUIWASHA TAA SWA63-1229M
(There Is A Man Here That Can Turn On The Light)

Ujumbe huu wa Ndugu William Marrion Branham, uliohubiriwa hapo awali katika Kiingereza mnamo Jumapili asubuhi, Desemba 29, 1963, katika Maskani ya Branham kule Jeffersonville, Indiana, Marekani, hapo awali ulitolewa kwenye kanda za sumaku na kupigwa chapa bila kufupishwa katika Kiingereza. Tafsiri hii ya Kiswahili ilichapishwa na kusambazwa na Voice Of God Recordings.

SWAHILI

©1989 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org